بِسْمِ اللَّـهِ الرَّحْمَـٰنِ الرَّحِيمِ

# KAZI NA BIDII NI NJIA YA MAENDELEO

*al-'Amal wa 'l-Fi'liyyah Tariq at-Taqaddum*


**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hassan Musa al-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul-Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba (Abulbatul)

ترجمة

# العمل
# والفاعلية
# طريق التقدم

تأ ليف
حسن موسى الصفار

من اللغة العربية  الى اللغة السوا حلية

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
Al-Itrah Foundation

**ISBN No:** 978-9987-17-029-6

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hassan Musa al-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba (Abulbatul)

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Mei, 2013
**Nakala:** 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@raha.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** w.w.w.alitrah.info

# YALIYOMO


Neno la Mchapishaji ........ v
Utangulizi ........ 6
Baina ya matarajio na Kazi ........ 9
  Matarajio na Uwelewa: ........ 9
  Fikra na Itikadi: ........ 12
  Kazi na mwenendo: ........ 16
Mahitaji ya Kazi ........ 19
  Upatikanaji wa vyanzo: ........ 21
  Nafasi za kazi: ........ 23
  Swali linalojitokeza lenyewe: ........ 25
  Jukumu la malezi: ........ 26
  Nafasi ya utamaduni: ........ 28
Kazi na bidii katika mtazamo wa Kiislamu ........ 33
  Kazi katika maisha ya Manabii na Maimamu ........ 38
  Imamu alikuwa anajituma wakati wote: ........ 39
  Mafunzo katika kupenda kazi: ........ 44
Wengine wanafanyaje kazi? ........ 49
  Mfano kutoka Korea ya Kusini: ........ 50
  Wajapani wanapenda kazi: ........ 51
  Maadui zetu ni mazingatio kwetu: ........ 54
  Uongozi wa Kimarekani: ........ 56
Sura ya wakati uliopita na wa karibu ........ 60
Ufanisi wa Kazi ........ 66
  Vipimo vya uzuri, ubora na ufanisi: ........ 71
  Vipi tutaamiliana na kazi? ........ 72
    1. Udhaifu wa raghba yenye ikhilasi: ........ 73
    2. Uwelewa duni wa kijamii na kiraia: ........ 75
    3. Kutokuwepo motisha: ........ 76
    4. Ukosefu wa uangalizi na usahihishaji ........ 76
    5. Athari ya mazingira yaliyopo ........ 77
Utamaduni wa ufanisi ........ 79
Malezi ya hukumu na mafunzo ........ 81
Mifano na vigezo ........ 83

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kwa jina la, al-*'Amal wa 'l-Fi'liyyah Tariq at-Taqaddum*, kilichoandikwa na Sheikh Hassan Musa al-Saffar. Sisi tumekiita, Kazi na bidii ni Njia ya Maendeleo.

Uislamu ni dini na ni mfumo kamili wa maisha. Kwa maana hiyo Uislamu mbali na kuwaendeleza waumini wake kiroho, huangalia pia na maendeleo ya waumini wake kimaisha katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na ustawi wa jamii kwa ujumla.

Ili mwanadamu apate kuishi maisha bora lazima afanye kazi. Uislamu unahimiza waumini wake kufanya kazi kwa bidii na ufanisi ili kuishi maisha mazuri kama yanavyoainishwa katika mafundisho ya Kiislamu.

Katika mfululizo wa vitabu vya mwandishi huyu, anahimiza waumini kuishi kwa kufuata mafundisho ya Kiislamu ambayo yanagusa kila uwanja wa maisha na kiroho. Katika kitabu hiki anazungumzia juu ya umuhimu wa kufanya kazi kwa mtazamo wa Kiislamu ili kupata pato halali kwa maendeleo yake ya maisha na hali kadhalika maisha ya kiroho.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kutoka na ukweli huu, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumini yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Abdul-Karim Juma Nkusui kwa kazi kubwa aliyofanya ya kukitarjumi kitabu hiki cha Kiarabu wa Kiswahili. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho vAkhera – Amin.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**
**Dar-Es-Salaam**
**Tanzania**

بِسْمِ اللَّـهِ الرَّحْمَـٰنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.**

وَقُلِ اعْمَلُوا فَسَيَرَى اللَّـهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ

**"Na sema: Tendeni vitendo Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Waumini wataviona vitendo vyenu."**
**(Suratu Tawba: 105).**

# UTANGULIZI

Mwanadamu ndio msingi wa kumea na ni kitovu cha harakati na mabadiliko, hayatopatikana maendeleo ya kweli isipokuwa kupitia kwa mwanadamu mwenye kujituma na hayatopatikana maendeleo isipokuwa kupitia katika jamii yenye mwamko, na nchi zetu na jamii zetu hazitoondokana na hali yake ya kutokuendelea isipokuwa watakapoamua watu wake kutumia uwezo wao na nguvu zao katika kazi na ujenzi. Je, mtu wetu amepungua chochote?

Hakika yeye hajapungukiwa akili na uerevu kuliko watu wa jamii nyingine, na vipaji vyake na utayari wake sio dhaifu kuliko wengine, lakini anachohitaji mtu wetu ni azma ya kazi, kuamua kujitolea kwa upeo wa nguvu yake na upeo wa

juhudi yake kwa ajili ya kujenga nchi yake na kutengeneza mustakabala bora zaidi.

Na azma ya kazi inamaanisha kuondoa vumbi la uvivu na uzembe, kupinga visingizio, kupambana na matatizo na ugumu, kuvumilia matatizo na taabu. Wengi kati yetu wanakosa azma hii na wanatoa hoja na nyudhuru mbalimbali na wanatupia lawama kwa wasiokuwa wao miongoni mwa pande na mazingira. Na wengine wanashangilia nafsi zao kwa kutoa juhudi ndogo au kubeba jukumu dogo.

Na azma ya kazi inapofunguka na kuchipua katika nafsi ya mwanadamu huwa inaakisi mionzi yake na athari zake katika nyanja mbalimbali za maisha yake, kwayo inafunguka akili yake juu ya miradi na mipango, na akili yake inazalisha rai na fikra, na zinachangamka hisia zake na viungo vyake kwa harakati na utekelezaji.

Na kwa kumiliki azma ya kazi na harakati inabadilika hali ya mwanadamu kiutamaduni, kiuchumi na kijamii. Hivyo kuenea kwa dini, kuipa nguvu sehemu yake na watu kuwa karibu na dini, mambo hayo hayapatikani ila ikiwa kuna kazi na harakati kutoka kwa wapambanaji kwa ajili ya mambo ya kidini. Pia kiwango cha utamaduni hakiendelei kwa mtu na jamii isipokuwa kwa kuwepo harakati za kiutamaduni na kiuchumi, bali ni kwamba mabadiliko na ukuaji haupatikani isipokuwa kupitia bidii na juhudi, na vivyo hivyo katika nyanja zingine.

Nimeishi na kutangamana na makundi mbalimbali na watu wengi miongoni mwa wanajamii, na nimewakuta wanalalamika juu ya upungufu na matatizo mbalimbali katika maisha yao, na wanazungumzia baadhi ya uelewa na matarajio katika nafsi zao, na licha yakuwa wanamiliki uwezo

mbalimbali na vipaji na zinapatikana kwao fursa nzuri na uwezo lakini wao wanaishia kulaumu na kulalamika, na kutoa hisia za matarajio na matumaini. Jambo ambalo lilikuwa linanisukuma kutafakari juu ya hali hii na kutafiti sababu zake na kiini chake na kutafuta njia bora na mbinu za kuweza kutoka katika hali hii kwenda kwenye wigo wa kujituma na maendeleo.

Kitabu hiki kidogo kwa asili ni hotuba nilizitoa katika baadhi ya minasaba. Na leo ambapo nazitoa ndani ya kitabu hiki nataraji zitachangia katika kutoa moyo wa kujituma na harakati, kukuza azma ya kazi na harakati zenye jitihada na juhudi, pamoja na kujua kwangu nyanja zingine zenye athari kubwa katika mas'ala ya harakati na kazi katika jamii yetu isipokuwa mimi katika mazungumzo haya naelekeza hotuba yangu kwa mwanadamu mwenyewe kwani akiamua kufanya kazi na akamiliki azma na akajipamba kwa tabia yake atakuwa ni mwenye kuweza kukabiliana na vizingiti na kuvuka vikwazo. Pengine Mwenyezi Mungu Mtukufu atatupa sote tawfiq katika kheri nakujitolea kwa ajili ya kufanya amali njema kwani Yeye ni Mwenye kusikia na ni Mwenye kujibu.

**Hasan Musa Saffar**
29 Julai 2000 – 27/4/1421 A.H.

# BAINA YA MATARAJIO NA KAZI

Kuna aina tatu za ulimwengu zinazouzunguka utu wa mwanadamu na zinatofautiana katika athari kutokana na uhalisia wa maisha yake, nazo ni:-

1. Ulimwengu wa matarajio na uwelewa.
2. Ulimwengu wa fikra na itikadi.
3. Ulimwengu wa shaka na kazi.

Na cha muhimu kwetu katika utafiti huu ni kueleza na kutafiti wigo wa mafungamano uliyopo kati ya mwanadamu na kila kimoja kati ya hayo matatu, na athari yake katika kutengeneza hali yake na mambo ya maisha yake.

## MATARAJIO NA UWELEWA:

Miongoni mwa mwanga wa nuru ya akili ambayo Mwenyezi Mungu ameifanya ni mahususi kwa mwanadamu, ni uwezo wa kufikiri na uelewa, hali anayoishi mwanadamu haimuwekei uzio wa fikra zake bali akili yake inapenya hadi upeo wa mbali, inavuka mazingira ya maisha.

Hivyo mwanadamu anasifika kwa hali ya kutafakari na kutamani, nayo ni zao la kipaji cha kuwaza, kwani anapowaza kitu anakitamani na anataraji kukifikia na anatafakari kukipata. Na mafanikio mengi ya mwanadamu ya kielimu na chumo lake la kimaendeleo mwanzo yalikuwa ni fikra, ndoto, dhana, matarajio na mawazo, hadi yakawa kwetu ni aina kati ya aina za adabu na fani, yanapewa jina la visa vya dhana ya kielimu, ambapo yanaitwa fikra kwa baadhi ya wanafasihi,

na kwamba yanaelea katika anga la dhana na matarajio, ili matukio yake yatengeneze mazingira na kupata hadhi ya uhalisia wa maisha na kuchora sura na mabango yanayovuka uwezo uliopo, lakini yanaweza kutokea baadaye na kuwa ni dhahiri hai yenye kuzoeleka.

Hakika kwenda angani na kusafiri kwenda mwezini ambapo mwanadamu amefanikiwa katika karne ya ishirini ilikuwa ni ndoto na fikra iliyopenya katika akili ya mwanadamu tangu karne ya pili, ambapo Msiryia Lusiyan aliandika kitabu kwa lugha ya Kiyunani kwa anuani ya "Qiswatu haqiyqiyyah" yaani kisa cha kweli.

Kama ambavyo baada yake Mfaransa Cyrano de Bergerac aliandika katika karne ya kumi na saba ndoto ya watu wakiruka angani kwa satalaiti na maroketi ya aina mbalimbali. Na mwanaanga wa Kijerumani Johannes Kepler akaandika kisa cha "Safari kuelekea mwezini."

Na ya kushangaza ni yale yanayotajwa kwamba vyombo vya usalama vya Kimarekani vilipatwa na shaka na bumbuwazi wakati mwandishi wa Kimarekani Kartimel alipochapisha kisa chake "Ahadi ya mwisho" mwaka 1944 ambacho kinaashiria utengenezwaji wa kombora la Nyuklia. Na sababu ya shaka hii na bumbuwazi hili ni kwamba wakati huo Marekani ilikuwa inajitahidi kutengeneza kombora la Nyuklia katika hali ya usiri mkubwa. Na ilithibiti katika utafiti uliofanywa na vyombo vya usalama vya Kimarekani kwamba mwandishi hakujua siri hii bali maelezo yake yalitokana na fikra zake na kazi ya dhana yake.[1]

---

[1]Al-Husein: Dr. Zaid bin Abdul – Husein: *Mubtakraatul-Aswir Waliydatul-Khayaal*. Jarida la Faiswal Uk: 4, Toleo la 222 la Mei 1995, Riyaadh.

Na juu ya upeo mpana wa uelewa wa mwanadamu na matarajio yake, Imam Ali bin Abu Talib (as) anasema: "Matarajio hayana mwisho."[2] Akasema pia: "Matarajio hayamaliziki."[3] Akasema tena: "Nafsi haiachi kutaraji hadi itakapoingia kaburini."[4]

Hakika matarajio makubwa ya mwanadamu hutimia pale anapokuwa mwenye kujituma na mwenye nguvu na bidii, na anapoandaa hali ya kujisukuma katika kazi, na kwa kiwango kile kile kazi huathiri maisha ya mwandamu mwenye kujituma katika mazingira yake.

Ama matarajio na uelewa unapogeuka na kuwa ni matamanio tu na ndoto za kipuuzi, mwanadamu anapotosheka kwa kujifurahisha kwa kupata picha yake katika akili yake na kujiburudisha kwa kuzikariri katika akili yake, matarajio hayo hayatakuwa na athari katika mazingira yake na hayatagusa chochote katika hali ya maisha yake.

Kutamani kitu peke yake bila ya juhudi katika kukifanya hakutakupa hata punje ya mafanikio ya kukifikia, Mwenyezi Mungu anasema:

أَمْ لِلْإِنسَانِ مَا تَمَنَّىٰ

**"Je, mtu anakipata kila anachokitamani?"**

**(Sura Najmi: 24).**

---

2 Ar-Rayshiahariy al-Muhammadiy katika *Mizanul–Hikmah* Juz. 1 Uk. 130, Maktabul – Iilaamil- Islaamiy, Qum 1403A. H.

3 Ar-Rayshiahariy al- Muhammadiy katika *Mizanul–Hikmah* Juz. 1 Uk. 130, Maktabul – Iilaamil-Islaamiy, Qum 1403A.H.

4 Ar-Rayshiahariy al- Muhammadiy katika *Mizanul–Hikmah* Juz. 1 Uk. 130, Maktabul – Iilaamil- Islaamiy, Qum 1403A.H.

Hiyo ni kwa sababu juhudi peke yake ndio njia ya kufanikiwa, Mwenyezi Mungu anasema:

وَأَن لَّيْسَ لِلْإِنسَانِ إِلَّا مَا سَعَىٰ ﴿٣٩﴾ وَأَنَّ سَعْيَهُ سَوْفَ يُرَىٰ ﴿٤٠﴾ ثُمَّ يُجْزَاهُ الْجَزَاءَ الْأَوْفَىٰ

**"Na kwamba hatapata mtu ila aliyoyahangaikia. Na kwamba mahangaiko yake yataonekana. Kisha ndio atalipwa malipo yake kwa ukamilifu."**

**(Sura Najmi: 39 – 41).**

## FIKRA NA ITIKADI:

Itikadi za kidini kwa mwanadamu humaanisha yale majibu ya maswali ambayo huwa mbele yake, ambayo huhusu uwepo wake na hatima yake na mwelekeo wake katika maisha haya. Wakati mwingine majibu hayo huwa ni matokeo ya uchunguzi na tafakari za ndani toka kwa mwanadamu, na wakati mwingine huwa ni matokeo ya kuiga, kufuata na mapokeo.

Hakika itikadi zinatofautiana, zipo zinazopatia ukweli na uhalisia, na zipo zinazokhalifu ukweli na uhalisia, na pia hutofautiana katika daraja la kupatia au kukhalifu.

Na ikiwa kufikia katika itikadi sahihi ni dharura na ni muhimu kwa mwanadamu basi yaliyo muhimu kwetu katika utafiti huu ni kuangalia jinsi itikadi hiyo sahihi inavy-

oathiri hali halisi ya maisha ya mwanadamu na mazingira yake. Kuamini itikadi sahihi haimaanishi kuzalisha hali sahihi daima na abadani, isipokuwa ni kwa kadiri itikadi hiyo inavyoakisi katika mwenendo wa mwanadamu na elimu yake. Qur'an tukufu inapozungumza juu ya imani inaiambatanisha mara nyingi na amali njema ili kuonesha mfano halisi wa imani na athari yake katika maisha ya mwandamu.

Mwenyezi Mungu anasema:

مَنْ آمَنَ بِاللَّـهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَعَمِلَ صَالِحًا فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ

**"watakao mwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na wakafanya amali njema, basi wao hawatakuwa na hofu wala hawatahuzunika."**

**(Sura Maida: 69).**

Amesema pia:

وَأَمَّا مَنْ آمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَلَهُ جَزَاءً الْحُسْنَىٰ

**"Na ama mwenye kuamini na akatenda mema tutamlipa malipo mazuri"**

**(Sura Kahf: 88).**

Amesema pia:

الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ طُوبَىٰ لَهُمْ وَحُسْنُ مَآبٍ

**"Wale ambao wameamini na wakafanya matendo mema, raha ni yao na marejeo mazuri."** **(Sura Ra'd: 29).**

Kutoachana huku baina ya imani na amali kumekaririwa katika zaidi ya aya sabini za Qur'an tukufu, hiyo ni ili kutilia mkazo ukweli muhimu, nao ni ulazima wa imani kuakisi kivitendo katika maisha ya mwanadamu na mwenendo wake, na kwamba haina thamani itakapokuwa ni nadharia tu iliyokomea katika fikra au ni matarajio yaliyoko katika nafsi tu.

Na haisihi abadani mwanadamu muumini kutaraji kuwa imani yake sahihi na itikadi yake sahihi itamsaidia katika kupanga maisha yake na kushika nafasi ya mwanzo kabla ya wengine bila uwezo wake na juhudi zake, kwani fursa ya kuendelea katika maisha iko kwa watu wote, na kanuni za Mwenyezi Mungu zenye hekima hazikubali upendeleo wala mahesabu tu. Hakika uwezo wa kuogelea baharini unamuokoa mwanadamu yeyote yule kutoghariki, sawa awe muumini au kafiri, ikiwa muumini hajui vizuri kuogelea basi atagharikí kwa kutekeleza kanuni ya Mwenyezi Mungu na wala imani yake haitamsaidia wala kuamini kwake kuokoka hakutomfaa, na ikiwa kafiri anaweza kuogelea basi atafika ufukweni mwa bahari kwa salama pamoja na ukafiri wake, Mwenyezi Mungu anasema:

كُلًّا نُّمِدُّ هَـٰٓؤُلَاءِ وَهَـٰٓؤُلَاءِ مِنْ عَطَاءِ رَبِّكَ ۚ وَمَا كَانَ
عَطَاءُ رَبِّكَ مَحْظُورًا

**"Wote hao tunawasaidia, hawa na hao, katika atia za Mola wako; na atia za Mola wako hazizuiliki."** **(Sura Israil: 20).**

Msaada wa Mwenyezi Mungu katika dunia sio mahususi kwa Waumini tu bali unatolewa kwao na kwa makafiri sawa kwa sawa, na hanyimwi yeyote kwa sababu ya ubatili wa itikadi yake au madhehebu yake. Imam Ali ibn Abu Talib (as) anawahutubia wale wanaotegemea nguvu ya kufikiri na kuhutubia huku wakiwa ni madhaifu katika kazi na harakati, anasema: "Hakika nyinyi mna haja zaidi ya utekelezaji wa kivitendo kuliko utekelezaji wa kauli."[5]

Pia anasema (as): "Utukufu mbele ya Mwenyezi Mungu ni kwa ubora wa vitendo na sio kwa uzuri wa maneno."[6]

Na katika vita vya Uhudi tunakuta ukweli ulio wazi wa usawa huu wa kimaisha na Sunna ya Mwenyezi Mungu, kwani pamoja na kwamba Waislamu wao ndio watu wa dini sahihi na itikadi ya kweli na kati yao alikuwepo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) naye ndio kiumbe bora zaidi wa Mwenyezi Mungu na anayependeza mno Kwake isipokuwa hilo halikuwasaidia katika kunusurika mbele ya maadui wa kikafiri wenye itikadi mbaya, pale Waislamu walipozembea katika

---

[5] At-Tamiymiy: Abdul-Wahdi al-Amadiy katika *Ghurar Wadurarail–Kalim*, Juz. 1, Uk. 262, Muasasatul –al-ilamiy –Beirut, chapa ya kwanza.

[6] Ariy shahariy al-Muhammadiy: katika *Mizanul-hikimah* Juz: 7 uk: 8 Maktabul-ilaamil – Islaamiy Qum chapa ya kwanza 1404 H

kazi na hawakujilazimisha na mbinu za vita ambapo watupa mishale waliteremka kutoka juu ya mlima na wakawapa maadui fursa ya kuwazunguka.

## KAZI NA MWENENDO:

Hakika juhudi ya mwandamu ndio hutengeneza hali yake katika maisha haya, na kwamba kazi yake na kujituma kwake ndio kunapanga daraja lake na kiwango chake cha maisha. Na tunapoona watu wanatofautiana katika viwango vyao, mtu binafsi, ummah na jamii basi kuna anayetengeneza ndani ya anga la kidunia la kimaendeleo, na kuna anayetumbukia katika mbinyo wa kutokuendelea, hivyo ni lazima tutafute sababu ya tofauti hii katika nyanja ya kimwenendo na kivitendo.

Kufaulu na kufeli, kuendelea na kutoendelea sio matokeo ya kutofautiana kiwango cha uelewa na matarajio wala sio athari ya itikadi na fikra tu bali ni hali ya kawaida ya matokeo ya kazi, kujituma na juhudi. Qur'an tukufu inasema katika aya mbili tukufu kwamba kazi ya mwanadamu ndio ambayo inapanga daraja lake na kiwango chake katika dunia na Akhera. Mwenyezi Mungu anasema:

وَلِكُلٍّ دَرَجَاتٌ مِّمَّا عَمِلُوا ۚ وَمَا رَبُّكَ بِغَافِلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ

**"Na wote wana daraja mbali mbali kutokana na yale waliyoyatenda. Na Mola Wako si Mwenye kughafilika na yale wanayoyatenda." (Sura Anam: 132).**

Na anasema pia:

وَلِكُلٍّ دَرَجَاتٌ مِّمَّا عَمِلُوا وَلِيُوَفِّيَهُمْ أَعْمَالَهُمْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

**"Na wote watakuwa na daraja zao mbali mbali kwa waliyoyatenda, na ili awalipe kwa vitendo vyao, na hawatadhulumiwa." (Sura Ahqaf: 19).**

Hakika daraja na kiwango cha kila mtu, mtu binafsi au jamii, haiji kwa kufikiria, kutamani na uelewa wake tu, wala kwa fikra zake na itikadi yake, bali ni "Kila mtu anatapata daraja kulingana na walivyofanya…." yaani daraja lake litapatikana kutokana na juhudi zake na kazi yake.

Hivyo ni juu ya mwanadamu aamini thamani ya kazi na juhudi yake kwani matakwa ya Mwenyezi Mungu katika ulimwengu yana hekima, yanatawala na ni ya uadilifu, hayaruhusu punje ya zao la juhudi na kujituma lipotee nje ya mizani na kanuni. Hiyo ni kwa sababu kupotea kitu kati ya juhudi na kazi hutokea ima kimakosa kwa sababu ya kughafilika na kutozingatia, na hii haipatikani kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na Mola wako si mwenye kughafilika kwa yale wanayoyafanya." Na ima kwa makusudi, na hiyo ni dhulma na kupunja, Mwenyezi Mungu ametakasika na hayo: "Na wao hawatadhulumiwa."

Hakika baadhi ya watu kwa sababu ya ujahili au kwa msukumo wa uzembe wanazembea katika Kazi na bidii kwa kushuku kwao umuhimu wa kazi na athari yake, am-

bapo wanapatwa na hali ya kupotoka na uvivu wa kujituma. Qur'an tukufu inawaambia hawa kwa msisitizo na ikionesha kosa la mtazamo wao na ikionesha hatima ya athari ya kazi yoyote anayoifanya mwanadamu katika maisha haya, hata ikiwa ni ndogo, iwe ya kheri au ya shari, Mwenyezi Mungu anasema:

أَنِّي لَا أُضِيعُ عَمَلَ عَامِلٍ مِّنكُم مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَىٰ بَعْضُكُم مِّن بَعْضٍ

**"mimi sitapoteza amali ya mfanya amali miongoni mwenu, akiwa mwanaume au mwanamke, ni nyinyi kwa nyinyi."** **(Sura Imran: 195).**

Na anasema:

فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٧﴾ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٨﴾

**"Basi anayetenda chembe ya wema, atauona! Na anayetenda chembe ya uovu atauona!" (Sura Zilzal: 7 – 8).**

# MAHITAJI YA KAZI

Jamii zetu bado zingali katika Ulimwengu wa tatu, zinakabiliwa na upungufu na kutokuendelea katika nyanja za maisha yake, miundombinu na mahitaji ya msingi bado hayajakamilika katika hatua mbalimbali tukiachilia mbali matumaini ya kujiunga na msafara wa maendeleo na kuingia katika uwanja wa jamii za kiviwanda zilizoendelea.

Inatosha kufahamu kwamba hata katika upande wa chakula, mahitajio ambayo ni kati ya mahitaji ya dharura sana ya kimaisha na sababu zake, pia kuna upungufu ulio wazi na nakisi kubwa. Makadirio yaliyoandaliwa na Taasisi ya Kiarabu ya kukuza kilimo yanatilia mkazo kwamba nchi za Kiarabu bado zingali zinategemea kuagiza sehemu muhimu katika mahitaji yake ya chakula cha msingi (Kama ilivyo Afrika), na kufuatana na takwimu zilizopo hakika nakisi katika uzalishaji nafaka inafikia kiasi cha tani 23 milioni kila mwaka, wakati ambapo kiasi cha kujitosheleza hakizidi asilimia 48, na inakadiriwa kima kinacholipwa na Dola za Kiarabu kila mwaka kwa kuagiza kiasi wanachohitaji katika nafaka toka nje ni kati ya dola bilioni 6 hadi 8 kulingana na mabadiliko ya thamani katika soko la dunia.

Na katika maelezo hayo hayo ni kwamba hakika uzalishaji wa Dola za Kiarabu katika sukari, nayo ni kati ya vitu vya msingi katika chakula hautoshelezi ila asilimia 36, ambapo pengo hilo hujazwa kutoka soko la dunia, nakisi hiyo ni kiasi cha tani 3.7 milioni kwa thamani kati ya dola 1.3 na 2 bilioni.

Na katika nyanja ya uzalishaji mafuta ya kula nchi za Ki-

arabu zinaagiza tani bilioni 1.750 kila mwaka ambapo kiasi cha kujitosheleza hakizidi asilimia 43.

Na katika makisio mengine ni kwamba ankara wanazolipa nchi za Kiarabu kila mwaka kwa ajili ya mahitaji yake kwa mazao yanayotokana na kilimo kwa vyakula vya msingi ni kiasi kinachokaribia dola bilioni 17 ambapo inaweza kuongezeka na kufikia dola biloni 60 kama itajumuisha gharama za kuagiza bidhaa za vyakula, nyama na samaki.[1]

Waziri wa biashara wa Misri Ahmad Juwayliy amesema wakati wa kufungua mkutano wa 34 wa kila mwaka wa muungano wa taasisi za biashara za nchi za kiarabu: “Hakika Dola za Kiarabu zinalipa kiasi kisichopungua milioni 40 kila siku kama thamani ya vyakula vinavyoagizwa kutoka nje, na mwanachi wa Kiarabu amekuwa anategemea nje katika kupata asilimia 65 ya mahitaji yake ya ngano, asilimia 74 ya sukari na asilimia 62 ya mafuta ya kula.”

Na akaongezea: “Hii inamaanisha kuwa nchi hizi za Kiarabu zimekuwa katika ujumla wake ni sehemu kubwa ya ulimwengu wenye upungufu wa chakula.”[8]

Na hali hii ya upungufu inazikabili ulimwengu wa Kiarabu na wa Kiislam katika nyanja na sehemu mabalimbali katika uchumi, elimu, teknolojia na utamaduni, ambapo tunaagiza sehemu kubwa ya mahitaji yetu kutoka nje.

---

[7] Al-Wasat: *Majalatu Usbuiyat*, London, toleo la 277 la tarehe 19/5/ 1997

[8] Al-Hayatu: *Jaridatu al-Yaumiyah*, London, toleo la 12415 la tarehe 17/10/ 1417 A.H.

## UPATIKANAJI WA VYANZO:

Lakini nakisi na upungufu huu sio kwa sababu ya ukosefu wa malighafi na uhaba wa uwezo, ukihesabu pato la mafuta, madini na sehemu nzuri za kijiografia ambazo zinapatiakana katika ulimwengu wa Kiislam na wa Kiarabu, kunapatikana uwezo mkubwa lakini aghlabu hauendelezwi vizuri kwa manufaa. Makisio ya kielimu yanasema kwamba Nchi za Kiarabu kwa sasa hazifaidiki na ardhi yake ya kilimo isipokuwa asilimia 10, ambapo kunufaika kwa mvua haizidi asilimia 15 wakati ambapo asilimia 38 ya maji yanapotea bure kutokana na uduni wa mifereji ya kumwagilia, kusambaza na kuvuja.

Na kwa mfano wa uwezo mkubwa ambao hauendelezwi tunaashiria juu ya ukweli uliochapishwa na jarida la al-Iqtiswad ambalo linatolewa na kitengo cha biashara na viwanda cha al-Mantiqatu as-Shariqiyat cha Mamalaka ya Kiarabu ya Saudia, ukweli uliochapishwa chini ya kichwa cha habari "Samaki ni utajiri upoteao", zifuatazo ni baadhi ya dondoo za maelezo ya habari hiyo:-

Sehemu za ghuba zinasifika kwa pwani pana ambayo ina upana wa kilometa 3500 kama ambavyo mwambao wake unachukua upana wa kilometa za mraba 250, na takwimu hizi zinaonyesha kwamba pato la samaki ni kubwa sana linalopatikana katika eneo hili pana la maji, na kwamba uwezekano wa kukuza pato hili kwa njia nzuri ni jambo linalowezekana.

Na Mamlaka peke yake ndio inamiliki mwambao mpana katika ghuba ya Kiarabu ambapo mwambao wake unafikia kilometa 2320 kati ya 1760 zilizopo katika Bahari nyekundu upande wa Magharibi na kilometa 560 za ghuba kwa upande

wa Mashariki. Na katika sensa kuna aina 180 za samaki na kamba katika maji ya Mamlaka.

Uzalishaji wa samaki katika mamlaka hadi mwaka 1993 umefikia tani elfu 50 nayo ni sawa na asilimia 50-65 tu ya matumizi, ambapo kiasi kinachoagizwa kimefikia tani elfu 28 mwaka 1994, hivyo kuna tofauti kubwa inayozidi asilimia 35 baina ya uzalishaji na matumizi.

Hakika nchi za ghuba hazizalishi isipokuwa asilimia 14 tu ya mali ghafi ambayo inaweza kuzalishwa kwa mwaka mzima, na imepelekea kutegemea ziada ya kuagiza bidhaa hizi muhimu za vyakula ambapo uagizaji wa nchi za Ghuba umefikia tani elfu 104 mwaka 1992.[9]

Na baadhi ya sensa rasmi zinaonyesha kwamba idadi ya wavuvi wa samaki (wenye kibali) inafikia 6848 katika Mantiqatu Shariqiy, kati yao 1019 ni Wasaudi, na wavuvi wa kigeni idadi yao inafikia 5829, wengi wao ni wafanyakazi wa kihindi, pamoja na kwamba kuvua samaki ni kati ya kazi za kienyeji katika sehemu husika.

Ukiachia mbali utajiri wa asili na uwezo mkubwa uliopo, pia kuna mali nyingi na fedha nyingi ambazo kwazo inawezekana kusaidia miradi ya uzalishaji, uendelezaji na utengenezaji, kwani kiwango cha mali za Waarabu zinazozalishwa nje zinakaribia dola bilioni 850 na uzalishaji katika Ghuba peke yake ni dola bilioni 350 katika soko la mali la kimataifa.

Na tunasoma katika ripoti ya faida ya matumizi na benki katika nchi zetu maelezo ambayo yanaonyesha ukubwa wa mtaji huo wa kifedha, na tija ya mali imedhihirisha kwamba faida ya maduka ya kubadilishia fedha ya Saudia na idadi

[9] Al- Iqitiswadi: *Majalatu Shahariyah*, toleo 272 la Novemba – Decemba 1995.

yake ni maduka 11, ambayo yametoa ripoti za kimali, imeongezeka hadi kufikia riyali bilioni 4.1 sawa na dola 1.7 bilioni katika nusu ya kwanza ya mwaka 1999.[10]

## NAFASI ZA KAZI:

Na kwa kuwepo uwezekano mkubwa, mali nyingi na ongezeko la idadi ya watu ambapo sensa rasmi inaashiria kwamba ongezeko hilo linafikia asilimia 4 kila mwaka katika Mamlaka, hakika nafasi za kazi zinapatikana katika nchi yetu kiasi cha kutosheleza mahitaji na kutoa huduma katika nyanja mbalimbali, hivyo nchi yetu inavutia mamilioni ya wataalamu na wafanyakazi, na kiwango cha kubadilisha fedha ambazo watumishi wa kigeni wa Saudia wamezituma katika nchi zao kimefikia zaidi ya dola bilioni 17 mwaka 1995, yaani ni sawa na asilimia 37 ya pato la Saudia la mafuta. Na wageni wanaoingia Saudia kwa ajili ya kazi ni zaidi ya milioni sita ambao wanatokana na mataifa 190. Na waziri wa mambo ya ndani wa Saudia amesisitiza kwamba Mamlaka ni kati ya nchi zinazoagiza wafanyakazi wa kike zaidi ulimwenguni. Na wafanya kazi wa kike wanaotoka ndani ya nchi katika sekta ya viwanda na taasisi maalum hawazidi asilimia 4 na katika nyanja ya huduma ni asilimia 12.[11]

Idadi ya wafanyakazi wanaume katika miradi maalum mwaka 1997 imefikia elfu 532 takriban, wakati wafanyakazi

---

[10] Al-Hayatu: *Jaridatu Yaumiyah*, la London, la 15/ 7 / 1999.

[11] Al-Wasat: *Usubuiya Siyasiyatu* la London uk: 38- 39 toleo la 203 la tarehe 18/12/ 1995

wa kike kutoka nje katika miradi hiyo katika mwaka huo huo wamefikia milioni mbili, na makadirio yanaonyesha kuna ongezeko la mahitaji ya wafanyakazi wa kike wa kigeni katika miaka inayokuja.[12]

Na tunaeleza kisa kifuatacho kama mfano wa kuwepo nafasi nyingi za kazi, ambapo idara zinazohusika Saudia zimegundua kwamba kuna mfanyakazi wa kihindi aliyeingia nchini kabla ya miaka 15 chini ya udhamini wa tabibu wa Kisaudia na akafungua kituo cha tiba cha kienyeji kwa timu ya wafanyakazi wa kihindi, matabibu, wauguzi, na wafanyakazi, na shughuli ikapanuka baada ya mafanikio ambayo ameyapata na amefungua baada yake zahanati huko Riyadh, Qaswim, Shariqiyah, Jiddah na Khamis Mushit, hadi jumla yake imefikia zahanati 18 anazoziendesha Mhindi husika, mfanyakazi huyu anaziendesha kwa kulipa riyali 2500 za malipo ya udhamini kwa Msaudia kwa kila zahanati, kila siku humwekea kiasi hicho katika akaunti yake ya benki bila Msaudia ambaye ndiye mdhamini wake kuingilia hesabu za faida, hasara, kodi ya majengo, maandalizi na mishahara ya wafanyakazi. Malipo ya udhamini ya Msaudia ya zahanati 18 yanafikia riyali milioni 1.3 kwa mwezi, wakati ambapo pato la mfanyakazi wa kihindi ni riyali milioni 1.8 kila mwezi.[13]

Vipi mfanyakazi wa kigeni anaanzisha zahanati 18 na anaziendesha kwa uhodari na kujituma na kupata faida kubwa wakati maelfu ya wananchi wanasongamana na wanazozona katika kazi zenye pato dogo, na wengi wanalalamika kwa ukosefu wa kazi na kukosekana nafasi za kazi?

---

[12] *Al-Yaumi*: la Damam toleo la 9621 la tarehe 18 Oktoba 1999

[13] *Al-Iqtiswad*: Jaridatu Yaumiyah la tarehe 11/2 / 1420 A.H. – 26/ 5 / 1999

## SWALI LINALOJITOKEZA LENYEWE:

Mbele ya wastani huu ambao unaelezwa na matukio na takwimu za kuwepo uwezekano mkubwa, mali nyingi, ongezeko la wakazi na nafasi kubwa za kazi, kwa nini nchi yetu bado ina upungufu wa kujitosheleza? Na kwa nini tunaagiza mahitaji yetu mengi toka nje? Bali ni kwa nini tunaishi katika hali ya kutokuendelea na upungufu wa mahitaji ya msingi katika maisha?

Na ambayo yanafanya swali liwe linasisitizwa zaidi ni ongezeko la ukosefu wa kazi katika nchi yetu kiasi kwamba imefikia asilimia 35 ya nguvukazi kulingana na baadhi ya ripoti, na imekuwa ni chanzo cha matatizo na hofu kwa viongozi na wananchi.

Ukosefu wa kazi katika nchi ambayo inaagiza zaidi ya wafanyakazi elfu sabini kila mwaka, na inahifadhi zaidi ya wafanyakazi milioni sita wa kigeni. Na imejaa nafasi nyingi za kazi ambazo zinakodolewa macho kuanzia baharini na sehemu inayoizunguka, hakika hali hiyo inaweka wazi juu ya upungufu mkubwa unaohusisha zaidi ya pande moja na sehemu zaidi ya moja, na inalazimu kutaka maoni ya jumla na kutangaza hali ya hatari katika nyanja za kisiasa, mafunzo, taasisi za uchumi, familia na malezi, maelekezo ya matangazo na utamaduni kwa ujumla.

Na katika utafiti wetu huu mazungumzo yetu yatakuwa juu ya sehemu muhimu na ya msingi katika uhalisia wa tatizo hili, nayo yanahusiana na kutengeneza azma ya kazi katika nafsi ya mwanadamu — mwanachi — na kumsukuma kuingia katika medani ya kujituma na kujishughulisha kwa bidii na jitihada kwa ajili ya kutengeneza dhati yake na ku-

dhihirisha vipaji vyake na uwezo wake, ili ashiriki katika kujenga nchi yake na kuinua jamii yake na umma wake.

## JUKUMU LA MALEZI:

Mwanadamu anakuja katika maisha haya kama malighafi, malezi na mafunzo yanafanya kazi ya kumtengeneza kinafsi na kitabia, hivyo hakika mafunzo halisi ya familia katika jamii yetu, tabia ya kuamiliana, malezi ya kizazi kinachoinukia na kutazama hali za maisha ambazo wanaishi watoto wa kizazi hiki katika utoto wao, hudhihirisha kwetu yaliyofichikana, mizizi ya mienendo yao, njia za kufikiri kwao na muamala wao pamoja na maisha.

Hali za maisha zilikuwa ni ngumu sana katika nchi yetu kabla ya miongo machache, zilikuwa zinasukuma familia katika maisha ya kujituma na kujishughulisha, mtoto alikuwa anafungua macho yake na kuona familia yake, wake kwa waume, wakubwa kwa wadogo wakiwa wanafanya Kazi na bidii ili kupata chakula cha kuishi na kuendesha mambo ya nyumbani, na hapakuwa na kitu chochote miongoni mwa njia za kujifurahisha au mazingira ya neema na utajiri isipokuwa katika wigo mfinyu sana.

Mtoto alileleka katika hali ya kujituma na kufanya kazi pamoja na familia yake kuanzia utotoni mwake, ambapo wazazi wanamchukua na anashirikiana nao katika baadhi ya kazi kama ambavyo binti anamsaidia mama yake tangu utotoni mwake katika kubeba majukumu yake na kazi zake za nyumbani.

Mtoto aliamka mapema kama wanavyoamka wazazi wake na alijifunza kazi chini ya uangalizi wao na alikabiliwa kama

wao na ugumu fulani na taabu na alileleka katika kubeba majukumu mapema katika umri mdogo.

Lakini maendeleo ya maisha ya kisasa yamelazimisha mabadiliko katika aina ya maisha ambapo yameandaa mazingira ya neema kwa kiwango cha kawaida, na mtoto hashuhudii tena chochote miongoni mwa taabu na kujituma katika maisha ya wazazi wake, wazazi wanafanya kazi zao mbali na mazingira ya nyumbani na mbali na familia, na akina mama wanatumia njia mabalimbali mbadala za vifaa vinavyofanya kazi haraka na bila ya taabu katika huduma za nyumbani bali wanasaidiwa na watumishi wa ndani na vibarua.

Na watoto wa kiume na wa kike wanaishi katika miongo miwili ya umri wao kama vile wageni watukufu, wanadekezwa na aghlabu wanahudumiwa katika nyumba zao wakati wa masomo hadi watakapojitegemea na kupata kazi.

Na baadhi ya familia zinavuka mpaka na hususan zenye utajiri hadi kuandaa mazingira mazuri na ya raha kwa watoto wao kwa kuwatimizia mahitaji yao ya kawaida tukiachilia mbali ya dharura na kuwapatia fedha nyingi mikononi mwao ili wazitumie bila ya kupata taabu yoyote ya kuchuma. Hali hii ambayo wanaishi watoto wa kizazi hiki katika kukua kwao kuanzia mwanzo wa umri wao, inaacha athari katika nafsi zao, athari ya kupenda raha na kuzembea katika kujituma na kujitaabisha.

Inanukuliwa kutoka kwa Waarabu wa Makka kwamba kabla ya Uislam walikuwa wanawapeleka watoto wao wadogo kwenye familia za mashambani jangwani ili wakajifunze kukabiliana na ugumu mbali na mazingira ya raha ya maendeleo na utajiri.

Hakika sisi inatupasa tuangalie katika malezi ya watoto wetu kwa kuwapa maandalizi ya yale yanayowasubiri miongoni mwa ugumu wa maisha, na tuwaandae kubeba majukumu ya kazi na kujenga taifa, na tuzingatie uwiano baina ya kuwapa raha na kuwahurumia kwao, na baina ya kutayarisha utu wao na kunoa azma yao na matakwa yao.

## NAFASI YA UTAMADUNI:

Mwanadamu anaweza kujituma katika kazi chini ya mbinyo wa haja na kupata mahitaji ya maisha, hivyo anajituma na kufanya kazi ndani ya mpaka huu, na anaweza kufanya shughuli na harakati kwa msukumo wa utamaduni na maarifa, wakati anapojua tabia ya maisha na kujua nafasi yake muhimu, na anapojali nafasi ya ummah wake na nchi yake kwa ujumla. Na hapa inalazimu kuwekeza katika wigo wa elimu na utamaduni, ili kutoka humo ipatikane nguvu na vikue vipaji vyake na uwezo wake, na mwanadamu atoe juhudi zake katika upeo na uwezo wake wa juu ili awe katika kiwango cha ushindani na mapambano baina ya ummah na maendeleo.

Jamii yetu na hususan kizazi kinachokua kinahitaji utamaduni wenye msukumo wa kazi na wenye msukumo wa mwelekeo wa kujitolea na kujituma. Na maelekezo ya kidini yana nafasi kubwa katika kutekeleza dauru ya msingi upande wa nyanja hii, kwa sababu dhana ya Uislamu na mafunzo yake inalenga kujenga utu wa mwanadamu mchapakazi mwenye kujituma ambaye ana uwelewa wa kuendeleza ar-

dhi na kuitumia dunia na kutekeleza ukhalifa wa Mwenyezi Mungu katika maisha haya.

Lakini tatizo ni yale yaliyotokea kwa baadhi ya wanadini baina ya kutenganisha maelekezo ya kidini na mambo ya maisha, ambapo matatizo ya maisha na mambo yake yamekosekana katika lugha ya mazungumzo ya kidini, mazungumzo ambayo yamekuwa yakijikita katika maelekezo ya mambo ya akhera na kuipata pepo na hurulain, bali baadhi ya watoa mawaidha na waelekezaji wamevuka mpaka hadi kiwango cha kuzima azma za watu juu ya kujituma na kufanya kazi, na hayo ni matokeo ya kusoma kimakosa baadhi ya dhana za kidini kama vile, dhana ya kujinyima dunia, uchamungu na kupenda mali na dunia, hivyo dhana hizi zinaonekana kana kwamba ni sababu za kupelekea kujitenga na masilahi ya kidunia na kupinga kupata chumo la kimaada.

Na huo ni upotovu ulio wazi juu ya msimamo wa Uislamu na kipimo cha mafunzo baina ya chumo la kidunia na thawabu za Akhera, kwani muumini wa kweli anaangalia maendeleo na kufaulu katika dunia na akhera na anasema kama alivyofundishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu:

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً

**“Mola wetu! Tupe mema duniani na (tupe) mema Akhera,”**
**(Sura al-Baqarah: 201).**

Na kama Mwenyezi Mungu anavyomuongoza:

وَابْتَغِ فِيمَا آتَاكَ اللَّـــهُ الدَّارَ الْآخِرَةَ وَلَا تنس نَصِيبَكَ مِنَ الدُّنْيَا

**"Na utafute kwa aliyokupa Mwenyezi Mungu makazi ya Akhera; wala usisahau fungu lako la dunia."**
**(Sura al-Qasas: 77).**

Na imekuja katika Hadithi tukufu: "Asiyekuwa na maisha hana marejeo."

Ama uchamungu, kujinyima dunia na dhana nyinginezo tukufu ni kama vile kemeo na vidhibiti kwa ajili ya kuratibu harakati za mwadamu katika maisha ili asitumbukie katika utelezi na maangamizi na wala asikose uzani wake au kufanya uadui kwa watu wajinsia yake.

Hakika aya za Qur'an tukufu na Hadith za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na Maimam watukufu miongoni mwa Ahlul – Bait wake watukufu (a.s) na wema kati ya masahaba wake, yote hayo ni maelekezo na msukumo wa juhudi na ijitihada, Kazi na bidii, bidii na harakati, na kwa muongozo wa maelekezo haya ummah wa Kiislamu ulitengeneza njia yake kuelekea kwenye maendeleo yenye kuchanua, na umetengeneza maendeleo yake yenye kuchanua na kunawiri, na ulipopatikana upotoshaji na udanyifu katika kueleza dhana ya Uislamu na fikra zake na hukumu zake, na sheria zake zikawa ni ibada tupu na mapokeo yasiyokuwa na roho yoyote, na wala hakuna harakati yenye kwenda sawia na hali ya maisha, hapo ndipo mwelekeo wa ummah ukarudi nyuma na maendeleo yake yakafifia na ukawa nyuma ya msafara baada ya kuwa unashikilia hatamu za uongozi.

Hakika sisi tuna haja kubwa sana ya kuondoa vumbi la kutokuendelea, vumbi ambalo limerundikana katika johari ya utajiri wetu na juu ya ukweli wa dhana za dini yetu, ili Uislamu urudi kama ulivyokuwa mwanzo, ukiwa ni mwanzilishi wa maendeleo na ujenzi wa maisha, na mwasisi wa mifumo ya harakati za kujitolea.

Na Maulama wa dini na makhatibu wa mimbari majukumu yao ni kutoa moyo wa Kazi na bidii, na kunoa azma ya uzalishaji na ubunifu. Baadhi ya Maulamaa wa dini na makhatibu wa mimbari wanaweza kujadili kwamba kazi yao ni kutoa waadhi na kuongoza na kufundisha hukumu za fiqihi na sio kuwahimiza watu juu ya kilimo au viwanda, na wala si kuwashajiihisha juu kuchuma masilahi ya kidunia, wanamimbari kama hawa ni juu yao kujongea katika maelekezo ya Hadith za Nabii na Maimam watukufu (as) ambao wamejihusisha na kila nyanja za maisha, kwa sababu hii tunakuta katika vitabu vya Hadith maelefu ya riwaya ambazo zinahimiza juu ya kazi na kushajiihisha juu ya kuchuma na kuelekeza katika nyanja za biashara, viwanda, ufugaji na mfano wa hayo.

Na vyombo vya habari ni wajibu vichukue nafasi yake kwa uzuri katika kuielimisha jamii, elimu itakayowasukuma wananchi kwenye uwelewa sahihi na matumaini endelevu, na viwaoneshe uzoefu wa wengine na upeo wa juhudi zao katika nyanja za elimu, teknolojia na viwanda.

Kinachosikitisha ni kwamba vyombo vingi vya habari badala ya kushiriki katika kutengeneza nafsi ya mwananchi katika msingi wa jitihada na majukumu na kujilazimisha, hakika vinasambaza utamaduni wa mmomonyoko na mporomoko wa kitabia na maadili, vinaeneza maisha ya ubadhirifu na

upuuzi nyuma ya matamanio na hawaa, na haviwaoneshi watoto wetu sura ya mapambano ya kielimu, kujituma na kufanya kazi kwa jitihada katika jamii iliyotangulia, bali vinatangaza filamu za ufisadi na upotovu ambao unapatikana huko na vinaleta udhaifu katika jamii.

Kama ambavyo mazingira ya jumla yaliyotawala katika jamii yetu, kwa mfano methali za kitaifa, habari mashuhuri na mazungumzo yenye kuenea katika mabaraza na vilabu, yanapasa kutia mkazo na kusisitiza juu ya kushajiihisha kujitolea kwa uzuri, na kuonesha uzoefu wa kielimu wenye kufaulu, na kuzijaza nafsi hali ya kupenda kazi na kuzipa raghaba ya kufanya kazi na kuvuka vikwazo na ugumu ambao unakwaza njia ya watendaji.

Na hakika hali tunayaiona katika baadhi ya jamii, ikiwa ni pamoja na kuenea hali mbaya, kudharau kazi hii au ile, kutokujituma, kutojitolea na kukuza upungufu na mianya ndani ya jamii, mazingira haya hakika ni kuimarisha uzorotaji wa jamii na ni kuzima azma na matakwa katika nafsi za watu wake na kudhuru mustakabala wao na maslahi yao.

Hakika baadhi yetu kwa ajili ya kudhihirisha hisia zao pamoja na huyu asiyekuwa na kazi au yule mwenye pato dogo, hakika utamkuta anawatupia lawama Maimam bila ya kumshajiisha mwanadamu huyu juu ya kubeba majukumu na kuongeza juhudi zaidi na kufanya jitihada, na kwa ajili hiyo inatawala mantiki ya visingizio na moyo wa kulaumu, kuvunjika moyo na kukata tamaa.

# KAZI NA BIDII KATIKA MTAZAMO WA KIISLAMU

Hakika Mwenyezi Mungu amemuumba mwanadamu katika maisha haya ili kujituma na kufanya kazi, kwani amepewa nguvu na uwezo, hivyo ni lazima kuutumia kwa bidii na jitihada, vinginevyo kuwepo kwake itakuwa ni bure na upuuzi kama ambavyo harakati na kujituma ni njia ya kuuzalisha uwezo wa mwanadamu na kukuza vipaji vyake, na bila ya hivyo utabaki umefichikana na unakabiliwa na changamoto ya kudumaa na kuyeyuka. Na kila juhudi ya mwanadamu inapozidi na kuongezeka harakati zake, ndipo unadhihiri uwezo wake na utu wake kuimarika kupitia juhudi zake na kazi yake, hivyo ni wajibu awe katika hali yake ya Kazi na bidii daima maadamu yuko hai, Mwenyezi Mungu anasema:

يَا أَيُّهَا الْإِنسَانُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَىٰ رَبِّكَ كَدْحًا فَمُلَاقِيهِ

**"Ewe Mtu! Hakika wewe ni mwenye kufanya bidii kwa Mola Wako, basi utamkuta."** **(Sura Inshiqaq: 6).**

Kinachotakiwa kwa mwanadamu ni kuutengeneza ulimwengu na kuendeleza kheri zake na neema zake, anga na nyota ambazo zinaelea angani na hazina iliyofichikana ndani ya ardhi, na utajiri ambao umejaa katika kina cha bahari, na uwepo wote huu wa ulimwengu mkubwa umedhalilishwa kwa ajili ya masilahi ya mwanadamu na umetayarishwa ili autumie katika mahitaji ya mwanadamu, katika nafasi ya

uongozi na utawala, akiwa kama khalifa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

## MWENYEZI MUNGU ANASEMA:

هُوَ أَنشَأَكُم مِّنَ الْأَرْضِ وَاسْتَعْمَرَكُمْ فِيهَا

**"Yeye ndiye aliyewaumba kutokana na ardhi na akaifanya iwe koloni lenu."** **(Sura Hud: 61).**

Na anasema:

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَكُمْ خَلَائِفَ الْأَرْضِ

**"Naye ndiye aliyewafanya makhalifa wa ardhi."**
**(Sura An'am: 165).**

Na kwa sababu hiyo inalazimu kutumia fikra na kutoa juhudi na kufanya kazi kwa wingi na kujituma ili kubeba majukumu ya ukhalifa na kuchukua nafasi ya kuamirisha ardhi na kuongoza, na hivyo tunakuta baadhi ya Hadith zinahimiza kazi na kuendeleza ardhi na kuleta uhai katika dunia, kama ile hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): "Hakuna Mwislamu anayepanda mmea au anayelima mmea huo kuliwa na ndege au mwanadamu au mnyama isipokuwa itakuwa ni sadaka kwake."[14] Na katika

[14] Al-Asqalaniy: Ibnu Hajar katika *Fatuhul-Bariy* Sharih ya *Sahihil-Bukhariy* Juz. 5 Uk, 5, namba 2320, Daru Salaam – Riyaadh Darul - Fayhai – Dimishiq, chapa ya kwanza 1997.

Hadith nyingine kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema: "Kama Kiyama kitasimama na katika mkono wa mmoja wenu kuna mche kama ataweza kuupanda basi asiinuke hadi aupande."[15]

Na kazi ndio lengo la ushindani baina ya wanadamu ili kupanga nafasi yao katika dunia na Akhera. Kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, kufaulu kwa kupata pepo yake na kupata ridhaa yake, hakupatikani isipokuwa kwa amali njema, na maendeleo katika dunia, na kupata chumo vile vile hakupatikani isipokuwa kwa njia ya kufanya kazi. Hivyo kazi ndio inayotengeneza hali ya mwanadamu katika dunia na Akhera.

وَوَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا ۗ وَلَا يَظْلِمُ رَبُّكَ أَحَدًا

**"Na wakakuta waliyoyafanya yamehudhurishwa. Na Mola Wako hadhulumu yoyote."** **(Sura Kahf: 49).**

وَنُودُوا أَن تِلْكُمُ الْجَنَّةُ أُورِثْتُمُوهَا بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ

**"Na watanadiwa kuwa hii ndiyo Pepo mliyorithishwa kwa sababu yay ale mliyokuwa mkiyafanya."** **(Sura A'araf: 43).**

Hakika jukumu la maisha ni kudhihirisha kipaji cha mwanadamu na uwezo wake katika njia ya ushindani katika kazi, Mwenyezi Mungu anasema:

---

[15] Al-Albaani: Muhammad Nasrudin katika *Silsilatul-Ahaadith as-Sahihah* Juz. 1 Uk. 11, namba 9, chapa ya nne 1985 al - Maktabu al-Islaamiy, Dimishiq - Beirut

الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۚ

**"Ambaye ameumba mauti na uhai ili awajaribu ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi."** **(Sura al-Mulk: 2).**

Na anasema:

إِنَّا جَعَلْنَا مَا عَلَى الْأَرْضِ زِينَةً لَّهَا لِنَبْلُوَهُمْ أَيُّهُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا

**"Hakika tumevifanya vilivyo katika ardhi kuwa ni pambo lake ili tumjaribu ni nani kati yao mwenye vitendo vizuri zaidi."** **(Sura Kahf: 7).**

## KAZI NI NGUVU NA KUJITUMA:

Mwanadamu anapofanya Kazi na bidii inaonekana kana kwamba ametumia juhudi zake na nguvu yake na kutumia wakati wake na raha yake, lakini kwa hakika wakati huo huo ambao anatoa anakuwa amechukua zaidi kuliko alichotoa. Hiyo ni kwa sababu Kazi na bidii ni chanzo cha nguvu ya kinafsi na kimwili.

Misuli ya mwanadamu na viungo vya mwili wake havipati nguvu kwa uvivu na ulegevu bali hakika hayo yanaupatia mwili unyonge na yanausababishia maradhi, na inaonekana katika zama hii vipi maradhi mengi yalivyoenea, kama vile unene, kolestrol, kisukari, romatizim na mengineyo ambayo

yanaitwa magonjwa ya kisasa yanayosambaa kutokana na uchache wa harakati za mwanadamu na udhaifu wa shughuli zake.

Na katika upande wa kinafsi: Hakika kazi inajaza faragha ya kinafsi ambayo inasababisha huzuni na hofu na kuongeza ari ya mwanadamu kupitia hisia zake, kwamba ana nafasi na tija. Kama ambavyo inamwongezea uwezo wa kuamiliana na mazingira, maisha na hali ya kijamii. Imam Ali bin Abu Talib (as) anasema: "Anayefanya kazi nguvu zake huongezeka na anayezembea katika kazi ulegevu wake huongezeka."[16] Na kuhusiana na athari ya kinafsi katika azi anasema (as): "Anayezembea katika kazi anakabiliwa na huzuni."[17]

Na kwa kuzingatia yale yanayozalishwa na kazi ikiwa ni pamoja na chumo kwa mwanadamu, hakika mrundikano wa mazao hayo humaanisha nguvu ya ziada katika hali ya mwanadamu. Na wanafalsafa wa karne za kati walikuwa wanasema: "Hakika kazi ina majukumu mengi kwa sababu ni lazima kwa mfanyakazi kupata chochote kwa upande mmoja, kama ambavyo ni lazima atengeneze dhati yake wakati anapofanya kazi kwa upande mwingine."

Na Mounier, kiongozi anayepigania utu Ufaransa alipozungumza juu ya nyanja nne za kazi hakika alikuwa anakusudia kwamba kazi inasawazisha hali ya nje na inatengeneza dhati zetu na inatukurubisha kwa watu na kuutajirisha ulimwengu wa maadili.

---

[16] Ar-Rayshahariy al-Muhammadiy katika *Mizanul-Hikima*, Juz. 7 Uk. 8, Maktabul- Iilaam al- Islaamiy Qum – chapa ya kwanza 1404 A.H.

[17] Rejea iliyotangulia.

## KAZI KATIKA MAISHA YA MANABII NA MAIMAMU:

Manabii na Maimamu walikuwa wanafahamu dini kuwa ni Kazi na bidii na walikuwa wanaifanya dini kama mfumo wa kujituma na harakati katika maisha haya, na wao ni kigezo ambacho ni wajibu mwanadamu Mwislamu aige kutoka kwao.

Walikuwa wanajua nafasi zao na fadhila zao kwa Mwenyezi Mungu na nafsi zao zilikuwa zimejaa maarifa yake na kumwamini, lakini wao hawakutegemea hilo na hawakutosheka na kuishia hapo bila kutoa juhudi na kubeba majukumu ya taabu ya kazi. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuwa alikuwa anasimama au anaswali hadi miguu yake au miundi yake inavimba, na akaambiwa juu ya hilo. Akasema: "Je nisiwe mja mwenye kushukuru?" Na katika riwaya nyingine. Aliambiwa: Kwa nini unafanya haya ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu na ambapo Mwenyezi Mungu ameshakusamehe madhambi yako yaliyotangulia na yajayo? Akasema: "Je, nisipende kuwa mja mwenye kushukuru?"[18]

Na imepokewa kwamba yeye (saww) alikuwa anasomba udongo siku ya Khandaq hadi tumbo lake likatoka jasho au tumbo lake likapata vumbi.[19]

Na Nabii anapokuwa nyumbani kwake hakuwa anakaa akiegemea na kustarehe akisubiri huduma kutoka kwa watu wake bali alikuwa anashirikiana na ahali zake kuhudumia

[18] Al-Asqalaaniy: Ibnu Hajar katika *Fathul-Baariy* Sharhi ya *Sahih Bukhariy* Juz. 8 Uk. 743, namba: 4836 Daru Salaam – Riyaadh, Darul- Fayhai – Damascus, chapa ya kwanza 1997

[19] Rejea iliyotangulia Juz. 7, Uk. 499, Hadith namba 4104.

nyumba, mke wake bibi Aisha aliulizwa ni kitu gani Nabii alikuwa anawafanyia ahali zake? Akasema: "Alikwa anashughulika na kazi wanayoifanya ahali zake, na unapokuja wakati wa swala anakwenda kuswali."[20]

Na katika riwaya nyingine kutoka kwa Aisha: "Alikuwa (saww) anashona viatu vyake, anashona nguo zake na alikuwa anaziba ndoo zake."[21]

Na bibi Khadija (as) amepokea kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuwa ulipoteremka wahyi aliacha kila raha na alikuwa anadumu usiku na mchana katika ibada na kazi. Nikamwambia: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hupumziki, hulali ?" Akasema: "Umeshapita wakati wa kulala ewe Khadija."[22]

## IMAMU ALIKUWA ANAJITUMA WAKATI WOTE:

Na Imam Ali ibn Abu Talib (as) naye ni mwanafunzi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), maisha yake na sira yake ni utekelezaji, Kazi na bidii katika pande na nyanja mbalimbali.

Katika upande wa ibada alikuwa anaitumikisha nafsi yake katika nyuradi na sunna hadi Ibnu Abil-Hadid al-Muutaziliy amesema juu yake: "Ama kuhusu ibada yeye alikuwa ni mwenye kuabudu sana kuliko watu wengine, mwingi wao wa swala

[20] Rejea iliyotangulia Juz. 10, Uk. 566, Hadith namba 6039.

[21] Rejea iliyotangulia Juz. 10 , Uk. 566, Hadith namba 6039.

[22] As-Shiraziy: Sayid Muhammad katika *Asabiylu Ilaa Nihaadhil-Musilimiyna* Uk. 147 chapa ya pili 1986 ya *Muasasatul-Balagh* - Beirut

na saumu, na kutoka kwake watu wamejifunza swala ya usiku, kudumu katika uradi na kuswali sunna, unadhani nini kwa mtu ambaye inafikia katika kuhifadhi kwake uradi wake al-itandika kipande cha ngozi huko Siffin usiku wa mapigano makali, akaswalia juu yake witiri yake huku mishale inaangukia mbele yake na inapita kwenye hema lake kulia na kushoto, haogopi kwa hilo wala hasimami hadi amalize kazi yake, na ni ipi dhana yako kwa mtu aliyekuwa paji lake ni kama vile ngozi ngumu ya ngamia kwa kurefusha sajda yake."[23]

Na katika upande wa maisha imepokewa kwamba yeye (as) aliacha huru mateka kutokana na juhudi ya kazi ya mikono yake.[24]

Na anasema mjukuu wake, Imam al-Baqir (as): "Amirul-Muuminina Ali bin Abu Talib (as) alikuwa anatoka wakati wa joto kali kwa ajili ya haja iliyompata, anataka Mwenyezi Mungu amuone anaihangaisha nafsi yake kwa ajili ya kutafuta halali."[25]

Imam Ja'far as-Sadiq (as) amesema kuwa babu yake Ali bin Abu Talib (a.s.) alikuwa anachimba visuguu na kutoa mchwa."[26]

Amirul-Muuminina Ali (a.s.) alikuwa anakata kuni, anafagia nyumba, na Fatimah (as) alikuwa anasaga, anakanda unga na kutengeneza mikate.[27]

---

[23] Ibnu Hadid: Abdul–Hamid katika Sharhi ya Nahjul–Balaghah, imehakikiwa na Muhammad Abul-Fadhil Ibrahim Juz. 1, Uk, 27, chapa ya pili 1965 ya Daru Ihiyai Turath al- Arabiy – Beirut.

[24] at-Tusiy: Muhammad bin Hasan katika *Tahadhibul-Ahkaami* Juz. 6, Uk. 326, chapa ya ya pili 1960 Matubaatu Nuumaan – Najaf.

[25] Al-Hurul Amiliy: Muhammad bin Husein katika *Tafswiylu Wasaailis-Shiah*, Juz. 17 Uk. 23, chapa ya kwanza 1993, Muasasatu Ahlil – Bait Liihiyai Turathi - Beirut

[26] Rejea ilitotangulia Uk. 37

[27] Rejea iliyopita Uk. 40

Amirul-Muumina Ali (as) anatoka akiwa amebeba mizigo ya mbegu za mitende, ghafla anaambiwa: "Ewe Abul Hasan nini hii iliyo pamoja nawe?" Anasema: "Mitende inshallah." Anaipanda na haufi hata mmoja.[28]

Hivyo Imam hakuwa anakula kitu kutoka katika Baitul-Mali bali chakula chake ni matokeo ya kilimo chake na kazi yake, anasema (as): "Hakika mimi naishi kwa yale yanayonijia kutoka katika chemchem na natosheka bila kuhitajia Baitul-Mali."[29]

Na katika kutilia mkazo hilo Imam as-Sadiq (as) anasema: "Ali (as) alikuwa hali isipokuwa yaliyopo hapa - Iraki – hadi aletewe kutoka Thamma - yaani Hijazi."[30]

Na Imam Ali (as) alikuwa anafanya kazi ya kununua mahitaji ya nyumbani kwake yeye mwenyewe kutoka sokoni na anabeba aliyoyanunua kwa sehemu ya shuka lake, na wakati mmoja watu walimuona na wakamuwahi wakamwambia: "Ewe Amirul-Muuminina sisi tukubebee." Akasema: "Mlezi wa familia ana haki zaidi ya kubeba mzigo wake." Na mara nyingi alikuwa anabeba tende na chumvi kwa mikono yake na anasema: "Mkamilifu hapungukiwi na chochote kutoka katika ukamilifu wake kwa kutenda yale yaletayo manufaa kwa familia yake."[31]

[28] Rejea iliyotangulia Uk. 41

[29] Al-Sharaqaawiy: Abdur- Rahman: *Ali Imamul-Mutaqiyna* Juz. 2 Uk. 28, chapa ya ya kwanza 1985 Muasasatul - Wafaa – Beirut.

[30] Al-Majilisi: Muhammad Baaqir katika *Biharul – Anwar*, Juz. 40, Uk. 325, Chapa ya pili 1983 Muasasatul - Wafaa - Beirut

[31] Al-Mudarisiy: Sayid Haadiy katika *Akhlaqiyaat Aamirul-Muuminin*, Uk. 114, Chapa ya kwanza 1991, Muasasatul - Iilaamiy ya uchapishaji – Beirut.

Na katika upande wa kijamii Imam Ali (as) alikuwa anajituma akijitolea kutumikia jamii na kuwasaidia watu mukabala na raha yake binafsi, na hakuwa anazembea katika nyanja hii, na kwa wakati wote hata usiku wa manane au katikati ya mchana, hata wakati wa jua kali.

Imepokewa kwamba Said bin Qais al-Hamdaniy alimuona wakati wa jua kali katika uwa wa ukuta, akamwambia: "Ewe Amirul- Muuminina unatoka katika saa hii?" Akasema (as): "Sikutoka ila kwa ajili ya kumsaidia aliyedhulumiwa au kumsaidia mwenye haja."[32]

Siku moja alireja nyumbani kwake wakati wa jua kali akamkuta mwanamke amesimama, mwanamke akasema: "Hakika mume wangu amenidhulumu, amenitisha, na amevuka mpaka kwangu na ameapa kwamba atanipiga." Akasema (a.s.): "Mja wa Mwenyezi Mungu subiri hadi jua lipoe, kisha nitakwenda pamoja nawe inshaallah." Mwanamke akasema: "Itazidi hasira yake juu yangu." Imam (a.s.) akatikisa kichwa akainama kisha akakinyanyua na akasema: "Hapana wallahi, inachukuliwa haki ya mnyonge bila ya ridhaa!"[33] Kisha akaondoka pamoja naye.

Na anapokea al-Asbagh bin Nabatah, naye ni kati ya wanafunzi wa Imam Ali (as), anasema: "Hakika Amirul-Muuminina alipokuwa Kufah alikuwa anaunganisha usiku na mchana, mchana na usiku kwa taabu, kukesha na kazi, anaswali na kufanya ibada usiku, kisha anaswali swala ya Asubuhi kisha anakaa baada ya hapo anasoma Qur'an

[32] Rejea iliyotangulia Uk. 178.

[33] Rejea iliyotangulia Uk. 185.

na kumsabihi Mwenyezi Mungu Mtukufu, na anasoma dua hadi linapochomoza jua, kisha anakwenda nyumbani kwake kwa muda kidogo, kisha anarejea ili kugawa wakati wake baina ya kwenda sokoni kwa ajili ya kuamrisha na kukataza na kutoa mawaidha na baina ya kwenda msikiti mkuu wa Kufah ili kukidhi haja za watu na kuhukumu baina yao katika sehemu inayoitwa Dukatul-Qadhaa, na inapofika Adhuhuri anaswali, na vivyo hivyo anafanya katika Alasiri hadi usiku na anaswali Magharibi, anaswali swala ya Isha na baada ya kupita theluthi ya usiku anakwenda nyumbani kwake.

"Siku moja nilikuwa pamoja naye ilipomalizika theluthui ya usiku, nilirejea pamoja naye nyumbani, nikalala uwani na Imam alikwenda kwenye chumba miongoni mwa vyumba vya nyumba na usingizi ulikuwa bado haujanijia basi nikamuona Imam anateremka kwenye ngazi naye ameinama kutokana na uchovu na kusinzia, na alikuwa anaegemea kwa mikono yake mitukufu kwenye ukuta, nikadhani kwamba Imam anataka kitu nikasema: 'Ewe Amirul-Muuminina unataka nini?' Akasema: 'Nataka kuswali baadhi ya rakaa kwa ajili ya Mola wangu.' Nikasema: 'Ewe Amirul-Muuminina muda mchache tu umeingia nyumbani? Na wala haujalala isipokuwa kidogo vipi unasimama huihurumii nafsi yako, hupumziki?' Imam akasema: 'Ewe Asbagh vipi nitalala? Nikilala mchana nitapoteza haki za raia wangu na nikilala usiku nitaipotezea nafsi yangu.'" [34]

---

[34] As-Shiraziy: Sayyid Muhammad katika *Asabiylu Ilaa Inhaadhul–Muslimiina* Uk. 148 chapa ya pili 1986 Muasastul - Balagh - Beirut.

## MAFUNZO KATIKA KUPENDA KAZI:

Na ikiwa watu wakubwa kawaida hupumzisha nafsi zao kutokana na uchovu wa kazi katika nyakati ngumu, hakika werevu miongoni mwa Waumini hawaachi kujitahidi na kujituma hata katika hali ngumu. Muhammad bin al-Munkadar anasema: Nilitoka kwenda katika baadhi ya sehemu za mji wa Madina katika wakati wa joto, nikakutana na Abu Ja'far al-Baqir Muhammad bin Ali bin Husein (as), na alikuwa ni mtu mnene akiwa amewaegemea vijana wawili au wafauasi wawili nikasema katika nafsi yangu: Subhanallah, mzee kati ya wazee wa Kikuraishi wakati huu na katika hali hii anatafuta dunia? Hakika mimi nitampa mawaidha, nikamsogelea nikamsalimia, akajibu salamu yangu kwa ishara huku akimiminika jasho. Nikasema: Mwenyezi Mungu akunyooshee mambo yako ewe mzee kati ya wazee wa Kikuraishi katika wakati huu uko katika hali hii kwa kutafuta dunia, unaonaje mauti yakikujia na wewe uko katika hali hii utafanyaje? Akasema: 'Lau mauti yakinijia na mimi niko katika hali hii basi yatakuwa yamenijia na mimi nikiwa katika utii wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, naizuia nafsi yangu na familia yangu kuomba kwako na kwa watu. Bali nilikuwa naogopa mauti yasije yakanifika na mimi nikiwa katika maasi kati ya maasi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.' Nikasema umesema kweli Mwenyezi Mungu akuhurumie, nimetaka kukupa mawaidha wewe lakini mawaidhi umenipa wewe."[35]

[35] at-Tusiy: Muhammad bin Hasan katika *Tahdhiybul-Ahkaami* Juz. 6 Uk. 325 chapa ya Nuuman – Najaf chapa ya mwaka 1960.

Hivi ndivyo anavyotupa Imam al-Baqir (a.s.) somo kubwa katika umuhimu wa kazi kwa mwanadamu vyovyote itakavyokuwa nafasi yake na utukufu wake na vyovyote itakavyokuwa hali inayomzunguka.

Na kuna kisa kinachofanana na hiki kinanukuliwa kutoka kwa mtoto wake Imam Ja'far as-Sadiq (as) kutoka kwa Abdul-A'alaa huria wa Aali Saam amesema: "Nilimpokea Abu Abdillah (as) katika baadhi ya njia za Madina katika siku za kiangazi zenye joto kali nikamwambia: Niwe fidia kwa hali yako mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na ukuruba wako kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na wewe unaitaabisha nafsi yako katika mfano wa siku hii? Akasema: 'Ewe Abdul-A'alaa nimetoka kwa ajili ya kutafuta riziki ili nijitosheleze bila kumuomba aliye mfano wako."'[36]

Na kazi kwa Mawalii haikuwa katika mpaka wa mahitaji tu bali ni ndani ya uwezo na kudra, maadamu unaweza kufanya kazi basi ni juu yako kufanya kazi hata kama huhitaji natija ya kazi au hata kama hupati natija yake. Kutoka kwa Anasi amesema: Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Kama Kiyama kitasimama na katika mkono wa mmoja wenu kuna mche akiweza kuupanda basi asisimame hadi aupande."[37]

Na inajulikana kwamba mche hadi kuwa mtende wenye kutoa matunda inahitaji miaka mingi lakini Mtume (saww) anamshajiisha anayeona Kiyama asisite kupanda mche wake pamoja na kwamba hatofaidika nao kwa chochote.

---

[36] at-Tusiy: Muhammad bin Hasan katika *Tahdhiybul- Ahkaami* Juz. 6 Uk. 325 chapa ya Nuuman – Najaf chapa ya mwaka 1960.

[37] al-Albaabiy: Muhammad Naswir din katika *Silsilatu al-Ahaadith as–Sahihah* Juz. 1 Uk. 11, Hadith namba 9 chapa ya nne al- Maktabul- Islaamiy 1985.

Amepokea Ibnu Jarir kutoka kwa Ammarah bin Khuzaimah bin Thabit amesema: Nilimsikia Umar bin Khattab anamwambia baba yangu: "Nini kinakuzuia kupanda ardhi yako?" Baba yangu akasema: "Mimi ni mzee nitakufa kesho." Umar akamwambia: "Nakuhimiza uipande." Hakika mimi nilimuona Umar na baba yangu wakiipanda.[38]

Na katika maelezo kuna riwaya nzuri kutoka kwa Imam Ja'far as-Sadiq (as) kutoka kwa Muhammad bin Adhafir kutoka kwa baba yake amesema: "Abu Abdillah alimpa baba yangu dinari elfu moja na mia saba akamwambia: 'Fanya biashara kwazo kwa ajili yangu.' Kisha akamwambia: 'Ama mimi hakika sina raghba na faida yake ingawa faida inapendwa lakini nimependa Mwenyezi Mungu anione ninanufaika na faida yake.' Baba anasema: 'Basi nikapata faida dinari mia moja kisha nikakutana naye nikamwambia: Nimekupatia faida dinari mia moja. Abu Abdillah akafurahi sana kwa hilo. Kisha akasema: Ziingize katika mtaji wangu.'"[39]

Imam as-Sadiq (as) anaashiria kwamba kazi ina athari katika kukuza fikra ya mwanadamu na rai yake na katika kukuza uwezo wake na vipaji vyake ambapo amesema mmoja wa wafuasi wake naye ni Maadh bin Kathir na alikuwa mfanyabiashara wa nguo, alitaka kuacha kazi sokoni kwa kutosheka na mali aliyokuwa nayo, akasema: "Nimeazimia kuacha soko na mikononi mwangu kuna chochote." Imam Ja'far akamwambia: "Hivyo itaanguka rai yako na wala chochote hakitakusaidia."[40]

---

[38] Rejea iliyotangulia Uk. 12

[39] Al-Huru Al-Aamiliy: Muhammad bin Husein katika *Tafswilu Wasaailus-Shiah* Juz. 17 Uk. 14, Namba 21859 Muasasatu Aali Bait Lil-ihiyai Turath – Beirut chapa ya kwanza 1993.

[40] Rejea iliyotangulia Uk. 329

Na katika riwaya nyingine Imam Ja'far alimuuliza sahaba wake Maadh bin Kathir: "Ewe Maadh umedhoofika kibiashara au umeiacha?" Nikasema: Sijadhoofika wala sijaiacha. Akasema: "Una nini?" Nikasema: Nina mali nyingi iko mikononi mwangu na sidaiwi na yeyote na wala sioni kama nitaila yote hadi kufa kwangu. Akasema: "Usiache biashara kwani kuiacha kwake kunaondoa akili."[41]

Na kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) amesema: "Hakika mimi najituma katika haja ambayo amenitosheleza kwayo Mwenyezi Mungu, siifanyi isipokuwa ni kwa sababu ya kutaka Mwenyezi Mungu anione najitolea katika kutafuta halali, je husikii kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Inapomalizika swala tawanyikeni katika ardhi na tafuteni fadhila za Mwenyezi Mungu…."**[42]

Hakika mwenye kuacha kazi na kutafuta uwezo, hakika yeye anatoa hoja yenye kuthibitisha kuwa hana sifa ya kheri katika nafsi yake. Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.) anasema: "Hakuna kheri kwa asiyependa kukusanya mali kwa njia ya halali."[43]

Na ikishindikana kwa mwanadamu katika baadhi ya nyanja za kazi ni juu yake asikate tamaa, atulizane na asiihukumu nafsi yake kwa kushindwa. Alikuja mwanaume kwa Imam as-Sadiq (as) akasema: "Hakika siwezi kufanya kazi kwa mikono yangu na wala sijui kufanya biashara na mimi ni mtu mwenye kuhitaji." Imam Ja'far (as) akamwambia: "Fanya kazi beba kwa kichwa chako na achana na kuwahitajia watu,

[41] Al-Hurul-Aamiliy: Muhammad bin Hasan katika *Tafswiylu Wasailus-Shiah* Juz. 17, Uk. 14, Namba 219859 Muasastu Aalil – Baiti Lil- ihiyai – Beirut chapa ya kwanza 1993.

[42] Rejea iliyoitangulia Uk. 28.

[43] Rejea iliyotangulia Uk. 33.

kwani Mtume wa Mwenyezi Mungu (as) alibeba jiwe juu ya shingo yake au begani mwake."[44]

Ali bin Abi Hamza amesema: "Nilimuona Abu Hasan – Imam Musa al-Kadhim (as) – anafanya kazi katika ardhi yake na miguu yake imetoka jasho. Nikasema: Nijaaliwe kuwa fidia kwako; watu wako wapo wapi? Akasema: 'Ewe Ali alifanya kazi katika ardhi yake kwa mikono yake yule aliyekuwa bora kuliko mimi na kuliko baba yangu.' Nikasema na ni nani huyo? Akasema: 'Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na Amirul-Muuminina (as), na baba zangu wote walikuwa wanafanya kazi kwa mikono yao, nayo ni kazi ya Manabii na Mitume, Mawasii na watu wema.'"[45]

Na kutoka kwa Abu Amru as-Shaybaniy amesema: "Nilimuona Abu Abdillahi (as) – Imam Ja'far as-Sadiq (as) – mikono yake ikiwa imeshika mwiko na juu yake kuna ubao mgumu anajenga ukuta wake na jasho linamiminika mgongoni mwake, nikamwambia: Niwe fidai kwa ajili yako nipe nikusaidie, akasema: 'Mimi napenda mtu ataabike kwa jua katika kutafuta maisha."'[46]

Na anasema Imam as-Sadiq (as): "Hakika mimi nafanya kazi katika baadhi ya mashamba yangu hadi nitoke jasho, hali ya kuwa ninaye anayeweza kunisaidia, ili Mwenyezi Mungu Mtukufu ajue kwamba mimi natafuta riziki ya halali."[47]

---

[44] Rejea iliyotangulia Uk. 38.

[45] Rejea iliyotangulia Uk. 39

[46] Rejea iliyotangulia Uk. 39

[47] Rejea iliyotangulia Uk. 39

# WENGINE WANAFANYAJE KAZI?

Hakuna siri iliyofichikana wala fumbo lisilojulikana wala sababu ya ghaibu wala athari ya kimuujiza ndani ya tofauti kubwa na mwanya mpana na wigo mpana unaotenganisha baina yetu na ulimwengu wa tatu, au nchi zenye kuendelea na baina ya nchi zilizoendelea au nchi za viwanda.

Sisi hatuna upungufu wa idadi wala uchache wa uwezo, tuna utajiri wa mazingira, wala hatulalamiki juu ya udhaifu wa uwezo wa kiakili na kiwango cha akili au vipaji. Hivyo ni kwa nini wengine wameendelea katika nyanja za elimu na viwanda na maendeleo ya sayansi na teknolojia, nasi tumebakia nyuma katika msafara wa kutokuendelea?

Imam Ali (as) anasema katika kuwakemea waliomzunguka juu ya uzembe wao kwa kulinganisha na kusongambele kwa maadui zao na ujasiri wao: “Mna nini, na nini dawa yenu, na nini tiba yenu, hali kaumu ni wanaume mfano wenu?!” [48]

Hakika hapa hatutaki kunyambua tatizo na kulifanya kuwa ni jepesi lakini tofauti muhimu iko wazi, nayo inazindua mtazamo wa mwenye kutafiti na kutafakari tofauti iliyopo baina ya hali yetu ya kutokuendelea na hali ya kuendelea kwa wengine, na tofauti hiyo kubwa ni kiwango cha kujituma na kufanya kazi na upeo wa kujituma na uzalishaji.

Katika nchi zilizoendelea kuna ushindani wa upendo katika nyanja ya Kazi na bidii, utamaduni na mafunzo, malezi na matangazo, taasisi na kanuni, na hali ya mazingira ya kijamii yote hayo yanasukuma kwenye kazi na uzalishaji, wakati am-

[48] Al – Musawiy: As-Sharifu Ridhwa katika *Nahjul- Balaghah khutuba*: 29

bapo nchi zinazoendelea kujituma kunapungua kwa kiwango chake cha chini kabisa na kuna visababishi mbalimbali na sababu nyingi za kudhoofisha moyo wa kazi na kuzima azma na kudumaza matumaini na ari, kukwaza hali ya kujituma na kushughulika.

Na hebu tutafakari baadhi ya ukweli juu ya hali ya Kazi na bidii iliyopo katika jamii zingine na tupime hayo kwa tunayoyaona na kuyashuhudia katika jamii zetu katika ulimwengu wa tatu.

## MFANO KUTOKA KOREA YA KUSINI:

Sifa makhususi na ambazo zimeitofautisha Korea ya Kusini ni bidii ya wananchi wake na uvumilivu katika kazi kwa kiwango cha kupigiwa mfano leo ambapo watu wanafanya kazi bila uzembe.

Na kwa sababu hii haikuwa ajabu uchumi wa Korea kuboreka na kutoka katika matatizo yake makubwa, ambao umeinawirisha nchi kwa sura ya haraka sana ukilinganisha na nchi zinazopakana nayo kwa upande wa Kusini mwa Asia ambazo zimepatwa na homa ya kuporomoka kwa sarafu yake, nayo ni matatizo ambayo mwanzo yalianzia Thailand.

Mashirika ya Korea yanahesabiwa kuwa ni mabigwa wa vipimo vya kimataifa na yanafikia mapato yake kiwango kinachovuka ukubwa wa wanayojifaharisha nayo nchi za Kiarabu zenye mafuta. Ama idadi ya siku za mapumziko ambazo wanazipata kila mwaka ni siku ishirini.

Hakika yote unayoyaona Korea kati ya magari ya aina mbalimbali, vifaa vya umeme na mengi wanayoyaonyesha

wauzaji ni utengenezaji wa viwanda vya ndani na ni vizuri vilevile.

Na haya yanatuongoza kwamba visingizio vya hoja za Waarabu zilizoenea havijafaulu katika kuizuia nchi mfano wa Korea isiweze kuendelea, yenyewe haina utajiri wa asili wenye kuinufaisha, na idadi kubwa ya Wamarekani waliopo katika nchi yao haijapunguza muono wao wa kienyeji na wa nje, na kuanguka sarafu yao ni katika matatizo mashuhuri na hayajabebwa na yeyote bali yamebebwa na Wakorea wote. [49]

Korea imetoka katika vita vibaya vyenye kuangamiza na vyenye mgawanyiko, na kwa wananchi wanaoishi kwa kilimo cha mpunga tu, haina petroli wala malighafi, kabla ya miaka 30 ilikuwa inasafirisha bidhaa ambayo thamani yake ni dola milioni 25, lakini imesafirisha kabla ya miaka miwili bidhaa ambayo thamani yake ni dola milioni 130 katika mazao ya uzalishaji wa viwandani.[50]

## WAJAPANI WANAPENDA KAZI:

Michel Alper mwanafikra wa Kifaransa ametaja katika kitabu chake *ar-Raasumaliyatu Dhidu Raasumaliyah*, kilichochapishwa Misri mwaka 1992 kikibainisha sensa kuhusu Japan, kinasema: Hakika asilimia 10 kati ya wanaume waliobalehe ambao wanakufa Japani kila mwaka wanajiua kutokana na wingi wa kazi. Na Wajapani wanapata wiki moja tu ya likizo ya mwaka.

---

[49] Rashid: Abdur Rahmani. *Jaridatu as-Shariq al-Ausat* la London 27/ 4/ 1999.

[50] As-Shirawiy: Yusufu Ahmad: Namba hizi tupu *Jariydatu as-Shariq al-Ausat* la London 28/4/ 1999

Serikali ya Japani imependekeza kupunguza saa za kazi kutoka saa 44 hadi saa 42 kwa wiki lakini wananchi wengi wanakhalifu pendekezo hili. Na waandishi wengi Japani wanaashiria juu ya hali ya mtu kufanya kazi maisha katika taasisi moja. Kuendelea kufanya kazi kwa muda mrefu katika taasisi ni jambo la dharura kwa anayetaka kupata mustakabala na kazi inayofaa.

Na imeonekana kwamba ujuzi wa miaka mitano tu katika taasisi maalum hauhesabiki kuwa ni ujuzi kwa hali yoyote ile, hususan mfanyakazi anapotaka kuhama kazi kwenda katika taasisi kubwa, akiwa hamiliki ujuzi wa muda mrefu hakika ni vigumu kwake kupata kazi katika taasisi zenye ushindani. Hivyo ama akubali kuhamia kwenye taasisi ndogo na zenye kiwango kidogo na zisizokuwa maarufu au kufanya kazi maalum ya binafsi. Na kwa hakika jamii haishajiishi mwenendo huu na hutafsiri kuwa ni kutokuwa na uwezo wa kujadili na kuelewana na wahusika au na taasisi aliyoachana nayo.

Na baadhi ya rejea zinaashiria kwamba dhana ya kazi kijamii kwa wafanya kazi wapya, humaanisha mnasaba wa kijamii na kifamilia ambao unastahiki sherehe kutoka kwenye shirika, sherehe ambayo hushiriki wanafamilia wa familia za wafanyakazi wapya. Na kwa sababu kufanya kazi katika mashirika huwa ni kwa msimu na kwa idadi kubwa, hakika familia inahesabu ni furaha iliyo sawa na furaha ya kuhitimu chuo kikuu kama inavyojulikana katika nchi zingine.

Na kwa kuwa kazi tangu mwanzo wake inafanywa kuwa ni tukio linalostahiki kusherehekewa, hivyo kuendelea na kazi inaonyesha ni mfanyakazi kuendelea kujiingiza katika duara la taasisi. Na hii inamaanisha kwamba mfanyakazi, taasisi na

familia ni alama ya mshikamano uliokamilika hakuna tofauti baina ya huyu na yule.

Hakika mfanyakazi haondoki tu kwa lengo kwamba yeye anafanya kazi kwa ajili ya kujenga familia au kwa ajili ya kuwafurahisha watoto wake kama baadhi wanavyosema, lakini pia ni kwa ajili ya kufaulu na kujenga taasisi ambayo anafanya kazi humo na kuleta maendeleo ya kiuchumi, hivyo kazi inakuwa ni ujuzi na ni sehemu ya kupatia riziki na kupenda, na hivyo wakati wa kazi sio taklifu kutoka katika taasisi bali ni mshikamano kutoka kwa mfanyakazi pamoja na kupenda kutimiza lengo la kuleta mafanikio.

Japani ni pwani tu iliyozungukwa na bahari na hali ya kijiografia toka kila sehemu, kushoto inamalizikia kwa ile iliyokuwa inaitwa Muungano wa Soviet na Saiberia ambapo ni eneo la baridi na sehemu ya kipeke na nadra kupatikana mwanadamu, inakaribiana na China upande wa Magharibi, nayo China ni nchi kubwa yenye kuimarika, idadi kubwa ya watu na maendeleo, ufahamu na mpanuko katika kila nyanja inapotaka, kwa kuwa ni nchi kubwa. Vivyo hivyo kwa Urusi au Muungano wa Soviet ya zamani. Tunaweza kusema hakika Japani ilikuwa na majirani lakini ni vigumu sana kuwa na jirani rafiki mpenzi muda wote. Ama pande zingine imezungukwa na bahari ambapo pepo na mawimbi ya bahari yanashindana kuipiga pwani ya Japani kwa kila upande. Ukichukua idadi yao ya milioni mia moja na ishirini na uchache wa rasilimali, tunajua kutokana na upembuzi huu wa haraka kwamba msongamano huu wa kijamii upo katika mapambano makali pamoja na mazingira, na katika mjadala mkali pamoja na rasilimali. Wingi wa wakazi ambao umeamua kuishi katika kiwango chenye kuendelea katika sehemu hiyo

unawajibisha kufanya kazi kwa ajili ya kuleta kiwango kizuri cha maisha.[51]

## MAADUI ZETU NI MAZINGATIO KWETU:

Waovu miongoni mwa Wayahudi walikutana toka sehemu mbalimbali za Ulimwengu ili wapore ardhi isiyokuwa yao na wakawafukuza watu wake kwa nguvu na mabavu kisha wakajenga dola ya kidhalimu wakaiita Israili na walitumia kila mbinu na hila ili kuwavuta walio mfano wao kutoka nchi mbalimbali, na karibu ididi yao imefikia milioni 5, wanaishi katika jamii kubwa ya kiarabu ya Kiislam inayokaribia bilioni moja na robo ya wananchi, na wote wanawatazama Wayahudi waliovamia na wanyang'anyi waliyopora, kwa mtazamo wa kupinga na wa uadui, na katika ardhi ya Palestina - waliyoiteka na kuipora hakuna utajiri wa kiasili wenye kuonekana.

Lakini hawa Wayahudi pamoja na upya wao na dola yao changa ambayo muda wake hauzidi historia yake ya nusu karne, na licha ya kwamba wao ni mchanganyiko usioafikiana, na kwamba mazingira yanayowazunguka ni ya hofu na yasiyo na utulivu, lakini wao wameweza kujenga katika dola yao nguvu inayoogopesha nchi za eneo hilo, inakwenda mbio kulitawala eneo hilo na wamepata mafanikio makubwa na mabadiliko ya kieleimu, kiviwanda na uzalishaji unaoshangaza.

Ni sahihi kwamba wao wanapata msaada toka Mashariki na Magharibi na hususan kutoka Marekani, lakini kwa usahihi msaada huu haukuja kwa ajili ya neema ya macho ya

[51] Az-Zaayir: Hasan Ali katika *Thulathiyatu at-Tatwibiyq al-Idaariy Fiy Yaabaani* 2 Novemba 1986.

Wayahudi bali ni kwa kuwa wao walilazimisha nafsi zao kwa juhudi zao na kujituma kwao, na anayesoma nafasi ya kikundi cha kiyahudi huko Marekani na Urusi anafahamu ukweli huu, kama ambavyo wao kwa juhudi zao waliweza kuuelewa msaada huu na wakaufasiri kwa kujenga nguvu na wakafaulu kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo katika kuimarisha uwepo wao wa kiuadui.

Waliiba na kunyang'anya ardhi ndogo lakini ni sehemu takatifu na ghali kati ya ardhi kubwa na pana sana za Kiislam, kisha wamejenga jengo lenye nguvu lenye kuendela kielimu, kiharakati na kujituma, wakati ardhi nyingi za Waislam na nchi zao wanakabiliwa na hali ya kutokuendelea na udhaifu wa kurudi nyuma. Vipi wanyang'anyi na wavamizi wanaweza kufanya harakati na kujituma katika ardhi isiyokuwa yao? Na ni vipi Waislamu wamedumaa katika nchi zao?

Moja ya takwimu inayotia uchungu inasema: Hakika pato la Israil yenye ubaguzi lilifikia dola milioni 78.1 mwaka 1994 na idadi ya wakazi wake ni milioni 5.4, wakati idadi ya wakazi wa Misri, Syria, Jordan na Palestina inafikia milioni 83.3 lakini pato lao wote ni chache kuliko pato la Israili.

Hapo kabla kwa miongo mingi Israil ilikuwa inahesabiwa ni moja ya nchi zenye kusaidiwa, yenye kupata msaada wa kimali toka asasi za kimataifa, lakini tangu mwaka 1976 yaani baada ya miaka 28 takriban tangu kuasisiwa kwake, inahesabiwa kuwa ni nchi iliyoendelea isiyostahiki mikopo ya Benki ya Dunia.

Na wastani wa uzalishaji wa jumla wa kila Mwisrail mwaka 1995 umefikia hadi dola za Kiamerika 16,000 nayo ni idadi inayoikaribia Uingereza ambayo inafikia dola 18, 700.

Na katika mwaka 1997 kulingana na maelezo ya waziri wa fedha wa Israili, uzalishaji wa jumla wa kila mtu kwa mwaka umefikia dola 17,000. Na baada ya muda wa kukua kukubwa ndani ya muda wa kati ya mwaka 1990 – 1996 ongezeko la uzalishaji limefikia asilimia 6 kwa sababu ya kujipanua katika nyanja zenye kukua ikiwemo sekta ya ufundi na elektoroniki.

Na kuna zaidi ya mashirika mia moja ya Kiisrail yamesambaa Burswah (Nasdaka) New York huko Marekani, mashuhuri kwa mashirika ya kiufundi ya hali ya juu, jambo linaloifanya kuwa dola ya kwanza katika idadi ya mashirika yaliyosambaa Marekani. [52]

## UONGOZI WA KIMAREKANI:

Uongozi wa Kimarekani (Elizabeth Cremieu Le Leadership American Dunnod Pars 1998, 128 page ), hiyo ndio anuani ya kitabu kilichotoka mwaka 1998, kina idadi kubwa ya takwimu na matukio ambayo yanazungumzia juu ya maendeleo ya kielimu, teknolilojia na maendeleo ya Marekani, jambo linalodhihirisha siri iliyopelekea nchi hiyo kuwa juu na kuutawala ulimwengu, na hata kama tukichukua tahadhari kuwa huenda lengo la kitabu hicho ni propaganda na kutangaza uongozi wa Kimarekani ulimwenguni, lakini hakika yaliyomo humo miongoni mwa takwimu, idadi na maelezo, yanalingana na uhalisia na hali iliyo wazi na maarufu katika ya maendeleo ya Marekani. Na mahala pa mazingatio katika hayo ni kwamba Waamerika hakika wamechukua nafasi hii

[52] *As-Sharq al-Ausat: Jaridatu Yaumiyatu* la London la tarehe 10/7/ 1999 Uk. 14.

kwa utendaji wa kazi, nayo ni nukta yenye nguvu inayokubali kupatikana.

Kati ya takwimu na maelezo ambayo kitabu kimeyapokea ni haya yafuatayo:-

Kati ya tuzo 450 za Nobel za kielimu zilizotolewa na idara ya elimu ya Sweden kati ya mwaka 1901 hadi 1996 Wataalamu wa Kimarekani peke yao wamepata tuzo 187.

Na kilimo cha Marekani ni kilimo cha kwanza duniani pamoja na kwamba hakiwakilishi isipokuwa asilimia 2.5 katika uzalishaji wa taifa la Marekani, na wala hakitumii isipokuwa asilimia 2.7 ya wafanyakazi wa Marekani. Pato lake la uzalishaji wa Soya ulimwenguni linafikia asilimia 48.9 na katika mahindi ni asilimia 40.3 na katika pamba ni hadi asilimia 19.4 na katika ngano ni hadi asilimia 10.7.

Na Ingawa soko la ndani linatumia asilimia 80 katika uzalishaji wa kilimo, hakika wakulima wa Kimarekani wao ndio wauzaji wa kwanza katika ulimwengu, mwaka 1996 hisa yao ya uzalishaji wa mahindi ulimwenguni ilifikia asilimia 75, na katika soya 69.8, na katika ngano asilimia 28. 3, na katika pamba asilimia 28.1.

Na licha ya kwamba umuhimu wa uuzaji wa mazao ya kilimo ya chakula ambayo katika mwaka 1995 yamefikia zaidi ya dola bilioni 50, lakini hayawakilishi isipokuwa asilimia 10 tu katika jumla ya uuzaji wa Marekani. Hivyo uuzaji wa Marekani unabakia kuwa ni wa kwanza katika uuzaji wa bidhaa za viwandani kwa zaidi ya asilimia 80.

Mashirika ya Kimarekani yanamiliki asilimia 50 katika soko la dunia la nafaka, na asilimia 73 katika uzalishaji wa bidhaa za viwandani, na asilimia 75 katika mauzo ya vipuri

vya runinga na utengenezaji wa vipuri vya ndege za kiraia na za kijeshi.

Na tangu mwaka 1990 uuzaji wa Marekani katika teknolojia ya kimataifa haukuacha kupata kasi ya maendeleo, kiasi cha mauzo ya katika nyanja hii yameongezeka kutoka dola bilioni 105 mwaka 1992 hadi kufikia bilioni 138 mwaka 1995, na kadiri ya shughuli za shirika la I. B.M la mashine za hesabu za elektoroniki peke yake imefikia dola bilioni 78.5 katika mwaka 1996.

Marekani leo inamiliki asilimia 40 ya soko la ulimwengu la mawasiliano, na soko hili peke yake mwaka 1996 limeuza zaidi ya dola bilioni 440, na Studio za Kimarekani zinamiliki karibu asilimia 80 ya picha zilizorushwa ulimwenguni, na zimeongezeka hisa za filamu za Kimarekani katika soko la Ulaya kati ya asilimia 56 mwaka 1985 hadi asilimia 76 mwaka 1994, na hii ni pamoja na udhibiti wa ulinzi ambao sekta hii imeuchukua katika baadhi ya nchi za Ulaya na ya kwanza ni Ufaransa ambayo baadhi ya viongozi wake hawasitisiti katika kuzungumzia tahadhari dhidi ya himaya ya utamaduni wa Kimarekani.

Na katika wakati ambao mashirika ya Kimarekani yanatawala humo kwa asilimia 80 hadi 90 katika soko la ulimwengu wa video na picha zinazorushwa, hakika inatumia utawala wake usio na kipimo cha idadi katika soko la maneno yenye kusomwa, hivyo wakala wa kwanza wa magazeti ulimwengu ni *The Associeted Press*, shirika la habari la Kimarekani. Shirika hili linatoa habari na picha 1.600 katika magezeti ya kila siku, na lina vituo 5.900 vya Radio na Runinga katika nyanja mbalimbali ulimwenguni, na kwa kweli sekta ya viwanda vya tasnia ya habari ni moja ya sekta zenye nguvu sana Mare-

kani, kiasi kwamba takwimu zinaonesha kuwa kazi za habari zimevuka pato la dola bilioni 220 katika mwaka 1994, huku ikipata asilimia 47 ya pato hili kutoka nchi za kigeni, wakati ambapo Marekani hawaagizi kutoka nje isipokuwa asilimia 2 tu katika matumizi yake ya utangazaji.

Uongozi wa kiutamaduni wa Marekani sio tu ni uongozi wa matangazo, kwani Marekani inapokea katika vyuo vyake vikuu na vyuo vingine vya juu kiasi cha wanafunzi wa kigeni 450,000, na wastani huu unaongezeka kila mwaka kwa wastani wa wanafunzi laki moja. Na wakati huo Marekani inauathiri ulimwengu kiutamaduni kupitia kundi hili la wanafunzi ambao husambaza utamaduni huo wanaporudi kwenye nchi zao, hivyo hupeleka katika nchi zao njia za kufikiria na ya kikazi za Kimarekani, na hakika vilevile inanufaika na kundi hili kwa kundi hili kuchangia kuendeleza miundo mbinu yake ya kiutamaduni ya ndani, kwani kuna makumi ya wanafunzi wa kigeni wenye kuhitimu kila mwaka katika vyuo vikuu vya Marekani ambao wanachagua kubakia daima Marekani, zaidi ya hapo ni ile sera ya uhamiaji iliyowekwa wazi kwa wageni walio watafiti na wenye elimu ya juu, hakika Marekani inaweza kuhesabiwa kuwa ni nchi ya kwanza yenye kufaidika na uhamiaji wa lazima katika ulimwengu wa leo.

Na mwisho inatosha tujue kwamba wakazi wa Marekani ni wachache kuliko asilimia 5 ya wakazi wa ulimwengu wote, lakini wao wanazalisha asilimia 25 ya bidhaa za dunia na kazi zake.

# SURA YA WAKATI ULIOPITA NA WA KARIBU

Uzembe wa kazi tunaoushuhudia na ulegevu na uvivu wa baadhi ya vijana wetu, je ni hali ya kurithiwa kutoka kwa mababa na mababu? Na je, vizazi vilivyopita katika nchi yetu viliishi katika hali ya kujidekeza, raha na maisha ya kitajiri kiasi kwamba hawakuzoea matatizo na taabu ya kujituma na kutafuta riziki?

Hakika maisha mapya katika jamii yetu ikiwemo raha na neema, hakika hiyo ni hali mpya isiyozidi umri wa nusu karne, na bila shaka bado tunaishi na watu ambao walikuwepo kabla ya muda huu wakiwemo mababa na mababu, hivyo ni juu yetu kuwauliza ili watusimulie kuhusu hali ya muda uliopita na vipi nyakati zake zilikuwa zinawalazimisha kujituma na kujishughulisha na zinawasukuma kuvumilia ugumu na matatizo. Walikuwa katika kiwango cha kukabiliana vikali na mazingira yanayowazunguka bali walijenga kwa ajili ya nafsi zao na jamii yao nafasi inayofaa inayosifika katika baadhi ya pande zake za kiuchumi na kijamii, hivyo walikuwa ni jamii yenye kuendelea, ilikuwa ni jamii yenye harakati za kujituma na zenye adabu, na ilikuwa na uzalishaji wa kilimo, kilimo ambacho kiliwapatia daraja kubwa ya kujitosheleza kichakula, huku harakati za kibiashara zikiwafanya kuwa ni kituo cha jamii za mashambani na vijijini.

Tunanukuu mazungumzo ya mmoja wa wanafasihi wetu watukufu[53] kuhusu baadhi ya hali za kujituma na kujishu-

[53] Sayid Ali Sayid Baaqir al-Awaamiy.

ghulisha katika wakati uliopita wa hivi karibuni ili iwe ni mazingatio kwa watu wa jamii ya kizazi hiki na iwe ni msukumo kwao katika kufuata njia ya mababa na mababu katika kujenga jamii yao, na kuipa nguvu nafsi ya nchi yao kupitia harakati zenye jitihada na kazi nyingi, nzuri, uaminifu, ikhlasi na kuwajibika.

Mfanyakazi katika kilimo alikuwa anaanza kazi yake tangu saa ya kwanza ya asubuhi wakati wa kuchomoza jua hadi mwisho wa mchana wakati wa kuzama jua, na hakuwa anafungwa na muda maalum wa kazi, ni sawa sawa awe anafanyakazi katika ardhi yake binafsi, au ni mfanyakazi katika bustani iliyo chini yake au ni mwajiriwa, utamuona anajituma katika kazi yake mchana kutwa. Hapumziki isipokuwa dakika chache ili kupata baadhi ya chakula, nacho sio zaidi ya baadhi ya matunda au tende pamoja na kiasi kidogo cha maziwa mgando na mkate, kisha anaendelea kujituma katika kazi yake kwa kulima (na jua kali) huku akifanya kazi ya kuimarisha ardhi na kugeuza udongo wake, au utamuona amebeba kikapu, zana ya kupandia mitende anahama toka mtende hadi mwingine ikiwa ni mwenye kufanya kazi ya mitende katika kuiotesha, kuipunguzia, kuipalilia n.k.

Kwa ujumla mkulima alikuwa anabakia kila siku na kwa mwaka mzima anafanya kazi mchana kutwa ili kujipatia yeye na familia yake chakula ambacho hakipatikani isipokuwa kwa kutoa juhudi kubwa na jasho la paji lake. Na sio mwanaume peke yake ambaye anajituma, kwani mwanamke naye pia anajituma mchana kutwa, pamoja na kwamba ana majukumu mengine ya nyumbani ya kulea watoto, kupika, kumhudumia mumewe na watoto wake, bado analisha ng'ombe, anamkamua na kuchuja maziwa kwa ajili ya kupa-

ta siagi, kama ambavyo anafanya kazi ya kuchuma matunda na kuokota yanayoanguka toka kwenye mitende miongoni mwa tende mbichi na mbivu. Pia kuna wanawake wengine wanafanya kazi ya kubeba matunda na kuyauza sokoni na kununua mahitaji ya nyumbani kama vile mchele, mboga na mengineyo bali na kununua nguo zake, za mume wake na za watoto wake, kama ambavyo mwanamke anafanya kazi ya kupeleka tende kwa mmiliki wake kwa kipindi chote cha kiangazi na kupeleka mafuta ya siku za Alhamisi za wiki za mwaka, na kupeleka maziwa na mengineyo mwezi mzima wa Ramadhani. Maisha ya mkulima yalikuwa tangu utotoni mwake hadi uzeeni mwake, yote hayo ni kujituma, kushughulika na kutoka jasho.

Na kuna kundi jingine la wafanyakazi ambalo tunaweza kulijumuisha na kundi la wakulima. Wao wanafanya kazi kwa njia ya kuhamahama na wanyama wakati huo, waswaga punda au waliokuwa wanaitwa "Waswagapunda", hawa hawaepukani na taabu na uchovu kama ndugu zao wakulima. Wao pia tangu asubuhi na mapema hadi jioni wanatembea kwenda na kurudi nyuma ya punda zao ambao wanabeba bidhaa mbalimbali juu ya migongo yao, wao ndio ambao wanaibeba toka chini na kuipandisha juu ya migongo ya punda, na wao ndio ambao wanafanya kazi ya kuishusha kutoka juu ya migongo ya punda na kuiweka katika sehemu zake zilizoandaliwa kwa ajili yake.

Pia kuna kundi la wafanyakazi mafundi. Hakika wao vilevile hawafungwi na saa maalum, ambapo kazi yao inaanza tangu kuchomoza jua hadi kuzama kwake, ni sawa iwe ni wakati wa kiangazi au masika, na wao wanafanya kazi ya kuvunja mawe na kuyahamisha toka sehemu hadi sehemu ya

kujengea, juu ya mabega yao na vichwa vyao, na wanapanda nayo ngazi ikiwa jengo ni la ghorofa kama ambavyo wanahamisha kokoto, mchanga na mengineyo.

Ama chanzo cha pili ni bahari. Hakika kazi humo inagawanyika katika sehemu nyingi, kuna kuzamia, kuvua samaki na kuna wanaofanya kazi kwenye meli za kubeba bidhaa baina ya vyombo vya ghuba. Na wote wanategemea katika kazi yao nguvu zao za kimwili, ambapo hawana njia yoyote ya kisasa inayowasaidia kuendesha meli ambazo wanafanya kazi humo. Na wazamiaji wako aina mbili:-

*al-Ghawsi* na *Sayib*: al-Ghawsi ni yule anayeteremka chini katika kina cha bahari ili kuchukua windo na wao wanakabiliwa na hatari za samaki wakubwa ambao wanakula binadamu kama vile nyangumi, papa na wengineo. Na Sayib ni yule anayekaa juu ya meli akishikilia kamba ambayo inaungana na mzamiaji ili amvute kutoka baharini ili kumwinua kwenye meli anapompa ishara. Na wazamiaji wanafanya kazi kwa muda wa miezi mitano ya kiangazi na wakati mwingine wanabakia mwezi mzima au zaidi katika bahari, na chakula chao ni samaki, tende na wakati mwingine ni wali.

Ama wale wanaofanya kazi ya kuvua samaki wao pia wanatoa juhudi kubwa mbele ya mitego yao na nyavu za kuvulia ili waweze kuzivuta na kuzinyanyua kwenye meli zinapojaa samaki. Au ambao wanakwenda kuvua kwa nyavu zao wanazibeba juu ya migongo yao na wanaingia baharini na hawana meli wala mashua bali wanabeba mifuko ya kuwekea humo samaki. Na kuna wale wanaokusanya samaki na kuwasomba toka kwenye mitego ya kujengwa baharini, ambapo wanakwenda katika mitego hiyo pale bahari inapoanza kupwa ili wakusanye yaliyomo ndani ya mitego hiyo zikiwemo samaki.

Hakika kazi zote hizi ni sawa ziwe za kilimo au kazi za baharini au kazi katika harakati zingine, zote zilikuwa zinategemea juhudi ya mwanadamu na nguvu zake na uwezo wake wa kimwili. Na hata ilipopatikana petroli na zikapatikana nyanja za kazi na ikahamia sehemu kubwa ya wafanyakazi katika sekta ya petroli, haikuwa ni kazi yenye raha na nyepesi katika miongo ya kwanza ya kuja kwa mashirika ya mafuta bali ilikuwa ni yenye kutaabisha na ngumu.

Wafanyakazi walipoanza kuelekea katika sehemu za kazi huko Dhaharani, vyombo vya usafiri havikuwa vimeenea kwa baadhi yao, na ni wachache walikuwa wanakwenda Dhaharani kwa kupanda punda, ama walio wengi walikuwa wanakwenda kwa kutembea kwa miguu masafa yanayozidi kilometa thelethini. Na hata baada ya wengi kujiunga na kampuni na wakakaa katika vyumba ambavyo vilijengwa na kampuni katika sehemu ya Su'ud (*Saudiy Camp*), walikuwa wanakabiliwa na mambo mawili, kwenda na kurudi kazini, hivyo ilikuwa ni juu ya mfanyakazi ambaye anaishi katika kambi aamke mapema na kwenda kwa kutembea kwa miguu kutoka kambini kwenda kazini, kiasi kwamba haifiki saa moja asubuhi ila huwa ameshafika katika sehemu yake ya kazi. Kisha anarejea kwa ajili ya chakula cha mchana kwa muda wa saa moja na nusu, na baada ya hapo saa kumi na moja jioni anarudi kwenye chumba chake. Hivyo ilikuwa ni juu ya mfanyakazi kutembea mara nne kwa siku, kupanda na kushuka, na kwa masafa mengi huku anakabiliwa na joto kali la kiangazi au baridi kali ya masika.

Na hata chumba pamoja na kuwa kina umeme lakini hakina kiyoyozi bali humo kuna panka. Lakini hizi panka hazisaidii kitu wakati wa joto la adhuhuri, ambapo chumba kilikuwa

kimejengwa kwa tofali hafifu na nje kuna rundo la mchanga unaopeperushwa na upepo hadi ndani ya vyumba maadamu milango au dirisha ziko wazi. Pamoja na taabu zote hizi wafanyakazi wa mwanzo wa Aramco walivumilia taabu na matatizo, na Aramco imesimama kwa juhudi za mikono yao na mabega yao. Uanzishaji wa shirika na wafanyakazi wake ulikuwa ni mfano wa ikhilasi na kujitolea katika kazi yao.

# UFANISI WA KAZI

Kipimo hakisimami katika mpaka wa kufanya kazi au kutokufanya kazi, kwani mahitaji ya maisha na haja zake zinalazimisha kwako mpaka wa Kazi na bidii, lakini kipimo chake ni kigumu mno na cha kina, kinatokana na ushindani katika kiwango cha kazi na daraja la ufanisi wake.

Ushindani mkali baina ya nchi za ulimwengu wa leo sio katika nyanja ya uwezo wa kuzalisha au idadi ya uzalishaji tu bali muhimu zaidi ya hayo ni bidii ya kushinda katika uzuri na ufanisi. Na kwa hayo vimeweza baadhi ya viwanda vya Kijapani ushindani wa kupigiwa mfano kuliko uzalishaji wa Kimarekani katika soko la Marekani. Na ikiwa ushindani wakati uliopita ulikuwa ndani ya duara na mpaka maalum lakini leo hii unakwenda kwa kiwango cha ulimwengu ambao umekuwa kijiji kimoja. Mzalishaji wa leo katika ubora na kiwango halinganishwi na aliye mfano wake, yule wa sehemu ya uzalishaji wake, bali anaingia katika mapambano ya ushindani pamoja na anayeshirikiana naye toka nchi mbalimbali za ulimwengu.

Kuanzia hapa unajitokeza umuhimu wa Qur'an tukufu kutilia mkazo katika kufanya kazi katika kiwango bora na kizuri zaidi na sio kufanya kazi tu katika kiwango chochote kiwacho.

1. Mwanadamu katika maisha haya amekuja ili kukabiliana na ushindani na maendeleo, Mwenyezi Mungu anasema:

إِنَّا جَعَلْنَا مَا عَلَى الْأَرْضِ زِينَةً لَّهَا لِنَبْلُوَهُمْ أَيُّهُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا

**"Hakika tumevifanya vilivyo katika ardhi ni pambo lake ili tumjaribu ni nani kati yao mwenye vitendo vizuri zaidi."** **(Sura Kahf: 7).**

Na anasema:

الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۚ

**"Ambaye ameumba mauti na uhai ili awajaribu ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi."** **(Sura al-Mulk: 2).**

2. Na mwanadamu muumini anapotaka kutoa fikra zake na itikadi yake kwa wengine na kuieleza kwao basi ni juu yake ajitahidi katika kuchagua mbinu bora na njia nzuri zaidi ya kutoa na kueleza, vinginevyo kueleza kwake kutakuwa dhaifu na kusikokinaisha au kubaya kunakowafukuza watu, Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَا تُجَادِلُوا أَهْلَ الْكِتَابِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ

**"Wala usijadiliane na watu wa Kitabu isipokuwa kwa njia iliyo nzuri kabisa;"** **(Sura Ankabut: 46).**

3. Na mwanadamu anapobeba majukumu ya kusimamia mali ya yatima asiyeweza ni juu yake asimamie idara ya mali yake kwa namna bora iwezekanavyo na kuikuza, Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ

**"Wala msiikurubie mali ya yatima isipokuwa kwa njia bora zaidi;" (Sura An'am: 152).**

4. Na mazungumzo ya mwanadamu pamoja na walioko pembezoni mwake ikiwemo kuwasemesha, haipasi iwe anavyotaka au kutokana na hasira zake na hisia zake, bali ni wajibu mwanadamu achague maneno mazuri zaidi na maana bora zaidi katika mazungumzo yake na wengine, Mwenyezi Mungu anasema:

وَقُل لِّعِبَادِي يَقُولُوا الَّتِي هِيَ أَحْسَنُ

**"Waambie waja Wangu waseme maneno mazuri."**
**(Sura Israil: 53).**

5. Na jumla ya muamala wa mwanadamu na ushirikiano wake na wengine ni juu yake ajitahidi ili aufanye uwe katika kiwango cha juu zaidi na kwa namna bora zaidi vyovyote itakavyokuwa misimamo yao kwake, Mwenyezi Mungu anasema:

ادْفَعْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ

**"Zuia uovu kwa lililo jema zaidi."** **(Sura Fussilat: 34).**

6. Na katika kuzatiti thamani ya ufanisi na kuinuka katika kazi na kwenda kwenye kiwango bora zaidi, hakika Qur'an tukufu inatia mkazo juu ya sifa hii ya kitendo cha kiungu na kilicho wajibu kwa mwanadamu, na si kingine isipokuwa ni kutafakari katika utukufu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, ili mtu aone kwamba kila kitu kimetengenezwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu katika upeo wa juu wa ukamilifu na ufanisi wenye ubora. Mwenyezi Mungu anasema:

صُنْعَ اللَّـــهِ الَّذِي أَتْقَنَ كُلَّ شَيْءٍ

**"Ni sanaa ya Mwenyezi Mungu aliyekitengeneza vizuri kila kitu."** **(Sura Naml: 88).**

Na anasema:

فَتَبَارَكَ اللَّـــهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ

**"Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji."**
**(Sura Mu'minun: 14).**

Na anasema:

الَّذِي أَحْسَنَ كُلَّ شَيْءٍ خَلَقَهُ

**"Ambaye ametengeneza vizuri umbo la kila kitu"**
**(Sura Sajda: 7).**

Na anasema:

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ

**"Hakika tumemuumba mtu katika hali nzuri mno."**
**(Sura Tin: 4).**

Na kwa lugha ya uaminifu Qur'an tukufu inatoa changamoto kwa wanadamu katika muda wa vizazi vyao vinavyoendelea ambao viwango vyao vya kielimu na teknolojia vinaendelea, waoneshe nukta ya udhaifu au kasoro iliyopo katika ukamilifu na uzuri wa ulimwengu huu mzuri ambao kila kiumbe kinanyenyekea humo katika mpango madhubuti. Mwenyezi Mungu anasema:

الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ طِبَاقًا ۖ مَّا تَرَىٰ فِي خَلْقِ الرَّحْمَٰنِ
مِن تَفَاوُتٍ ۖ فَارْجِعِ الْبَصَرَ هَلْ تَرَىٰ مِن فُطُورٍ ﴿٣﴾ ثُمَّ
ارْجِعِ الْبَصَرَ كَرَّتَيْنِ يَنقَلِبْ إِلَيْكَ الْبَصَرُ خَاسِئًا وَهُوَ حَسِيرٌ

**"Aliyeumba mbingu saba kwa matabaka. Huoni tafauti yoyote katika uumbaji wa Mwingi wa Rehema. Hebu rudisha jicho! Unaona kosa lolote? Tena rudisha jicho mara mbili, jicho lako litakurudia likiwa dhalili lililochoka."**
**(Sura Mulk: 3 – 4).**

# VIPIMO VYA UZURI, UBORA NA UFANISI:

Kwa ushindani mkali katika kusukuma uzalishaji na umuhimu wa ubora na ufanisi ulimwenguni, kumekuwa na vyama na taasisi za kupanga sifa za ubora, na kutoa ripoti jinsi sifa hizo za ubora zinavyolingana na bidhaa zinazozalishwa, na sasa limepatikana shirika linalojulikana kama (Izu 9000), nalo ni shirika la viwango vya ubora.

Na miongoni mwa nchi zilizo mbele katika kuzingatia ufanisi katika sifa za vipimo vya ubora ni Japani, wanasema kwamba uzingativu huu kwao umepitia hatua tatu za kihistoria:-

Hatua ya kwanza: Ni kuanzia mwaka 1955 hadi mwaka 1965. Katika kipindi hiki walitilia mkazo ubora wa kila mwaka kwa kupunguza kiwango cha makosa na mianya katika uzalishaji, kwa mfano katika uzalishaji wa sukari ubora unakuwa kwa kupunguza kiasi kikubwa cha uchafu kiasi kwamba kiasi cha uchafu kinakuwa asilimia 10 au 5 na yanayofanana na hayo. Hivyo viwanda vinashindana katika kupunguza kiasi cha makosa.

Hatua ya pili: Kuanzia mwaka 1965 hadi 1975 waliondoka katika hatua ya kukosekana kosa kiasi kwamba uzalishaji unakuwa sahihi kwa asilimia mia moja.

Hatua ya tatu: Baada ya 1975 nayo ni hatua za ubora wa aina, kiasi kwamba ushindani wa uzalishaji wa kupata kiasi kikubwa zaidi cha alama za ziada za ubora. Hakika kazi kutokuwa na upungufu na kasoro ndio kiwango cha chini kabisa cha ufanisi na ubora wake, lakini kuna viwango na vipimo vingine ambavyo hivi sasa vinachukuliwa kwa uma-

kini na uzingativu, na miongoni mwa vipimo hivyo ni upeo wa uharaka wa kufanikisha, unaweza kupata mbele yako bidhaa nyingi zenye kulingana sifa, lakini zatofautiane katika upande wa wakati wa kufanikisha na kukamilisha, na hiyo huwa ni sifa ya upendeleo na ya ziada yenye matumizi machache ya muda. Kama ambavyo pia uboreshaji na kuongeza sifa za ziada ndio lengo la ushindani katika ubora na ufanisi katika nyanja mbalimbali za kazi na uzalishaji.

## VIPI TUTAAMILIANA NA KAZI?

Katika nchi zetu inatolewa mizania kubwa, na wakati mwingi na juhudi kubwa zinatumika katika miradi na utekelezaji wa kazi katika sekta binafsi na za kiserikali, lakini matokeo aghlabu ni udhaifu wa uzingativu, uangalizi duni, ubora duni wa kazi na ufanisi duni usioridhisha, na kwa sababu hiyo mianya na kasoro zinakuwa nyingi katika miradi, na hatimaye unachelewa ufaulu wake kama ambavyo kazi nyingi hazitoi matokeo yaliyotarajiwa, na baadhi ya uzalishaji unafeli katika medani ya ushindani wa bidhaa zinazoagizwa.

Wakati mwingine tunatumia mizania kubwa kwa ajili ya kuweka lami barabara na mitaa, na baada ya muda zinaharibika na kuchakaa, na tunajenga ghorofa au nyumba kwa kiasi kikubwa cha fedha lakini baada ya muda mfupi inadhihiri kasoro na upungufu. Na tunasoma kwa mfano katika jarida la Misri baada ya muda na muda kuporomoka kwa baadhi ya ghorofa, na mashamba ambayo hayana muda mrefu tangu kuanzishwa kwake. Kuna makosa mengi ya kitiba katika hospitali mbalimbali na taasisi zetu za afya. Vivyo hivyo tunakabiliwa katika nyanja mbalimbali na kiwango kidogo cha

uazalishaji na kazi, ingawa hatuwezi kukusanya takwimu zote lakini kuna mabadiliko na mafanikio ya kujivunia. Lakini ni mafanikio finyu ukilinganisha na hali ya jumla iliyoenea katika nchi za ulimwengu wa tatu.

Hakika wengi wetu wanafanya kazi vyovyote itakavyokuwa bila ya kuzingatia ubora na ufanisi. Na huenda sababu na vyanzo vinavyojitokeza, vinavyoleta hali hii ni hivi vifuatavyo:-

### 1. Udhaifu wa raghba yenye ikhilasi:

Ambapo baadhi wanafanya kazi zao kana kwamba wamelazimishwa, hivyo haupatikani kwao msukumo na raghba ya ndani katika kufanya kazi, hivyo wanaifanaya kwa uzito na uvivu na kama alivyosema Imam Ja'far as-Sadiq (as): "Uvivu unaidhuru dini na dunia."[1] Na amesema (as): "Adui wa kazi ni uvivu."[1]

Na Mwenyezi Mungu (swt) anawalaumu wanafiki katika swala zao kwa sababu wao hawazitekelezi kwa ikhilasi na msukumo bali ni kwa uzito na uvivu, Mwenyezi Mungu anasema:

وَإِذَا قَامُوا إِلَى الصَّلَاةِ قَامُوا كُسَالَىٰ

**"Na wanapoinuka kwenda kuswali, huinuka kivivu."**
**(Sura Nisaa: 142).**

[54] Al-Hakimiy: Muhammad Ridhwaa Ali katika *al-Hayatu* Juz. 1, Uk. 301.

[55] Al-Hakimiy: Muhammad Ridhwaa Ali katika *al-Hayatu* Juz. 1, Uk. 299.

Hakika mwanadamu katika kazi yake anatumia juhudi yake na wakati wake, hivyo ni kwa nini anadharau ambayo yanateketeza dhati yake? Na kwa nini anakubali kupoteza nguvu yake na juhudi yake katika kiwango cha chini chenye kuporomoka?

Ni kweli hakika mwenye kuheshimu nafsi yake anaheshimu kazi yake na kwamba anayethamini juhudi yake na wakati wake anazingatia ufanisi wa utelekezaji wake na uzalishaji wake.

Na katika mtazamo wa Kiislam hakika Kazi na bidii katika kuendesha mambo ya maisha ni jambo tukufu, nayo iko katika daraja la ibada bali katika daraja la jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, kwani imepokewa kutoka kwa Imam Ja'far as-Sadiq (as): "Mwenye kujituma kwa ajili ya familia yake ni kama mpigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu."[56]

Na amepokea Anas bin Maliki kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliporejea kutoka katika vita ya Tabuk alipokewa na Saad al-Answariy, akampa Nabii mkono kisha Mtume akamwambia: "Ni nini hii ninayoiona katika mkono wako (yaani sugu ngumu)?" Saad akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu nalima na kumwagilia kisha naitumia katika kuhudumia familia yangu." Mtume wa Mwenyezi Mungu akabusu mkono wake na akasema: "Mkono huu hautaguswa na moto."[57]

Hakika mtumishi, mfanyakazi na mtu anayejituma, mwanachuoni na khatibu, anapotoka kwenda kazini kwake kwa

---

[56] Al-Kulainiy: Muhammad bin Yaaqub katika *Al-Kaafiy*, Juz. 5, Uk. 88.

[57] al-Falsafiy: Muhammad Taqiy katika *Ashabaab Bainal-Aqil Wal-Atifah*, Juz. 2, Uk. 311 - 312.

shauku na raghaba basi ataamiliana pamoja nayo kwa ikhilasi na kuitekeleza kwa ubora na ufanisi.

## 2. Uwelewa duni wa kijamii na kiraia:

Sote tunakosoa na tunadhihirisha kuchukizwa na kiwango duni cha uzalishaji na utekelezaji wa kazi katika jamii yetu, lakini kiukweli ni kwamba tunazichukia nafsi zetu wenyewe na tunazilaumu nyendo zetu wenyewe, kwa sababu sisi ni washiriki katika kutengeneza hali hii ya uduni, kila mmoja katika nafasi yake na kupitia dauru yake na kazi yake ni mshiriki katika uduni huu.

Wakati mmoja niliwasikia baadhi ya wananchi wanalalamikia kitendo cha mmoja wa wafanyakazi kushindwa kutekeleza kazi za Marja'a kama ipasavyo, na ikatokea baada ya muda nikakutana na mfanyakazi huyo huyo akieleza malalamiko yake dhidi ya mfanyakazi aliyehitaji kumuona katika sehemu nyingine ya kazi, nikasema: *Subhanallah!* hakuna mmoja wetu anayehisi uzembe wa mwingine katika upande wake na wala yeye hahisi upungufu wake kwa wengine? Anaona kasoro inapoakisi katika masilahi yake moja kwa moja na anaghafilika kwayo anapodhuru masilahi ya wengine?

Hakika kutengeneza na kubadilisha hali ya jamii yetu kunaanzia kwa kila mmoja wetu, kwa sababu kila mmoja anapasa kutekeleza dauru fulani, hivyo akitekeleza kwa ufanisi dauru yake atakuwa amechangia katika kutatua sehemu ya upungufu, na anakuwa ni mfano kwa wengine na anashajiisha juu ya hayo.

### 3. Kutokuwepo motisha:

Jamii ambazo zinazingatia ubora na ufanisi zinanyenyekea kwenye kanuni adilifu zilizowekwa zinazoheshimu vipaji, na zinatia msukumo kwa kutoa vitu vinavyotia moyo kwa wenye bidii na wazalishaji wenye ufanisi zaidi. Na hiyo ni sababu muhimu kwa ajili ya mageuzi na maendeleo.

Ama unapotawala wastani wa hisabu na ubaguzi baina ya wahusika, huku upendeleo na ufisadi ukisambaa, bila shaka idara hiyo itakuwa ni kiwanda cha kuuwa uwezo na mageuzi, na mtumishi atakuwa butu katika juhudi zake na nguvu zake ikiwa hakupata heshima na ujira au akiona huduma yake inapelekea masilahi ya wakuu wake na viongozi wake tu.

### 4. Ukosefu wa uangalizi na usahihishaji:

Kwa sababu ya kuficha makosa na kufumbia macho kasoro na upungufu, na kutawala mazingira ya kujipendelea na upendeleo, yote hayo yanaimarisha hali ya kupuuza na kuzembea na uduni katika kazi na uzalishaji.

Hakika taasisi za uangalizi, upelelezi, njia za habari, mazingira huru ya ushindani mkali, na uelewa wa watu unaowawezesha kutambua tofauti iliyopo baina ya mzalishaji huyu na mwingine na baina ya raia huyu na mwingine, huleta athari ya mwangaza wa wazi katika kugundua kasoro, mapungufu na makosa, na ni msukumo wa kuelekea katika utatuzi na usahihishaji.

Mwanachuoni wa dini, khatibu, mfanyakazi na wasiokuwa wao, anapohisi kila mmoja wao kwamba dauru yake na uzalishaji wake, uko chini ya kiwango na ubora, na kwamba

anashukuriwa na anaheshimiwa na kuhisaniwa anapofanya vizuri zaidi na kwa ufanisi, na anaadhibiwa anapofanya vibaya na kuzembea, hakika atakuwa na uzingativu zaidi na kuchunga kiwango cha elimu yake na uzalishaji wake. Ama ikiwa hajaona kitu miongoni mwa hayo na kwamba kila kitu "kinaenda" kulingana na maneno yaliyoenea, matokeo yake yanayotegemewa ni hali hii mbaya iliyoenea.

## 5. Athari ya mazingira yaliyopo:

Mwanadamu anapoishi ndani ya mazingira salama chini ya utaratibu na kanuni, na kutawaliwa na hali ya nidhamu na ufanisi, hakika aghlabu huelekea katika mazingira hayo na huamiliana pamoja na hali iliyopo. Na anapozungukwa na mazingira na hali mbaya hupotoshwa na mazingira hayo mabaya. Na tunawasikia watu wengi wakianza safari za kazi zao kwa kuwajibika na kwa nidhamu katika taasisi au nyanja ambazo wanajiunga nazo, lakini hawakai muda mrefu, ghafla huanza kupoteza hali nzuri na wao wanakuwa ni sehemu ya hali mbaya na upotovu. Sababu ya hayo ni kuathirika kwao na kuamiliana kwao na hali ya mazingira waliyoyakuta na yanayowazunguka. Jamii yetu imeishi na uzoefu hai juu ya hili katika sehemu za Mashariki katika Mamlaka ya Kiarabu ya Saudia, na mfano halisi katika upande huu unaonekana katika hali ya nidhamu na uwajibikaji ambao unatawala kazi katika shirika la Aramco tangu kuasisiwa kwake, ambapo wafanyakazi wameleleka humo katika hali ya kudhibitiwa na wakati wa kazi bila ya kuwepo uzembe wala uchelewaji, na pia katika hali ya kudumu katika kazi bila kughibu hata katika hali ngumu sana, huku wakifunzwa ufanisi wa kutekeleza majukumu na kazi kwa umakini na kwa mpangilio. Hapo

mwanzo wafanyakazi wengi walikuwa hawajui kusoma, wasio na elimu na wala hawakuwa wanamiliki ujuzi wa fani vya kutosha, lakini idara makini na iliyoratibiwa katika shirika ilitengeneza mazingira na hali yenye udhibiti na ufanisi, kupitia ufanisi huo wafanya kazi wameleleka katika ufanisi na uzalishaji bora.

# UTAMADUNI WA UFANISI:

Jamii inahitaji maelekezo mengi na utamaduni wa jumla unaosukuma kwenye ufanisi, na mwanadamu atekeleze kazi yoyote anayoifanya hata kama ni ndogo kwa umakini, nidhamu, utaratibu na uzingativu.

Na kwa sababu hiyo zimepokelewa riwaya na Hadithi za kidini ambazo zinatilia mkazo juu ya tabia hizi muhimu. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema: "Hakika Mwenyezi Mungu anapenda anapofanya kazi mmoja wenu aifanye kwa ufanisi."[58]

Na katika Hadith nyingine kutoka kwake (saww): "Hakika Mwenyezi Mungu anapenda kwa mtumishi anapofanya kazi aifanye vizuri."[59]

Na tukio la Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kushiriki katika kumzika Sahaba mtukufu Sa'ad bin Maadh linatupa sisi maelekezo mazuri katika kujilazimisha umakini na ufanisi, ambapo imepokewa kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliteremka hadi katika mwanandani wa Sa'ad bin Maadh na akasawazisha udongo juu yake na akawa anasema: "Nipatie jiwe, nipatie udongo, nipatie udongo mbichi" na anaziba kwa udongo huo mianya, na alipomaliza akafukia udongo juu yake na akasawazisha kaburi lake, akasema (saww): "Hakika mimi najua kuwa atapata mtihani na itamfikia balaa

---

[58] al-Hindiy: Hasaam Diyn al-Mutaqiy katika *Kanzul-Ummal*, hadith namba: 9128.

[59] al-Hindiy: Hasaam Diyn al-Mutaqiy katika *Kanzul- Ummal*, hadith namba: 9129.

lakini Mwenyezi Mungu anampenda mja anapofanya kazi aifanye kwa ufanisi."[60]

Namna hii Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anatilia umuhimu muundo wa mwanandani na kaburi licha ya kwamba hatarajii manufaa yoyote kwa muundo huo na kwamba muundo huo utaishia kubomoka siku za baadaye, lakini kinachotakiwa ni kuzingatia hali hii ya ufanisi na ubora katika mwenendo wa mwanadamu.

[60] ar-Rayshahariy Muhamaadiy katika *Mizanul-Hikimah*, Juz. 7, Uk. 29.

# MALEZI YA HUKUMU NA MAFUNZO:

Na tunapotafakari mafunzo ya kidini na hukumu za kisheria ambazo zinafungamana na ibada na mikataba na tukatazama umakini wake katika ufafanuzi na kuenea kwake katika nyanja mbalimbali zinazoambatana nazo tunakuta zinaunda madrasa ya malezi, zinamfunza mwanadamu Mwislam umakini na nidhamu na zinamlea katika kujali ufanisi, nidhamu na ubora.

Kwa mfano maudhui ya kujisaidia na kuondoa uchafu katika mwili, jambo hili pamoja na kudharaulika kwake na wepesi wake kwa mwanadamu, katika sheria ya Kiislam lina makumi ya mas'ala na hukumu baina ya wajibu, haramu, makuruhu na mustahabu, ili mwanadamu atekeleze amali hii ya kibaiolojia ya kawaida kwa njia bora zaidi, na bila ya nyongeza yoyote na bila kusababisha madhara juu yake, kwa wengine na kwa mazingira.

Na katika kitabu kimoja kati ya vitabu vya Hadithi nacho ni *Tafswiylu Wasailus-Shiati Ilaa Tahaswiyl Masailus-Shariah cha* Mwanachuoni Sheikh Muhammad bin Hasan al-Hurru al-Amiliy aliyefariki mwaka 1104 Hijiria kuna Hadith 174 kuhusu maudhui ya kujisaidia.

Na ibada ya Swala ambayo Mwislamu anaitekeleza mara tano kila siku imenadhimiwa kwa idadi kubwa ya hukumu na vidhibiti, ikiwemo sehemu yake, nafasi yake, harakati zake, matamshi yake na vazi lake ambalo analivaa ndani yake, masharti na utangulizi na vigawanyo, kiasi kwamba Shahi-

di wa kwanza Muhammad bin Jamali Diyn Makiy al-Amiliy aliyezaliwa mwaka 734 - 786 Hijiria, alihesabu akakuta kuna wajibu elfu moja katika Swala, wajibu alizoziorodhesha ndani ya kitabu kinachoitwa *al –Alifiyyah*.

Haikubaliki kutekeleza Swala kwa aina yoyote na vyovyote inavyokuwa bali ni lazima kuchunga miiko yake na hukumu, vinginevyo kasoro na kupuuzia kwa makusudi kwa sharti lolote au sehemu ya swala hata kama ni herufi moja, kunabatilisha Swala na kuifanya kuwa ni upuuzi. Na mambo ni vivyo hivyo katika ibada ya Saumu na faradhi ya Hija.

Mwisho tunaashiria katika Hadithi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuhusu kumhalalisha mnyama na kumchinja kwake, mafunzo na adabu ambazo inapasa kuzichunga katika nyanja hii ambapo anasema (saww) katika aliyoyapokea Muslim katika *Sahih* yake: "Hakika Mwenyezi Mungu amefaradhisha wema katika kila kitu, mnapouwa basi uweni kwa uzuri na mnapochinja chinjeni kwa uzuri, na mtu anoe kisu chake."[61]

[61] *Sahihi Muslim.*

# MIFANO NA VIGEZO

Hakika kwa kila mwelewa katika jamii na hususan anayekuwa katika nafasi ya utawala na uongozi aifanye nafsi yake kuwa mfano na kigezo katika nidhamu ya kazi na ufanisi wake, wazazi wawili katika nyumba wanaathiri kwa mwenendo wao katika kutengeneza nafsi za watoto na tabia zao. Baba mwenye kuratibu katika maisha yake na mwenye kuwajibika kwa umakini katika kazi yake, kwa kawaida tabia zake hizi zinaakisi katika shakhisiya ya watoto wake. Na mama ambaye anaendesha sehemu ya mambo ya nyumbani kwa mpangilio na ufanisi aghlabu wanamuiga watoto wake katika nyendo zao kwa mwelekeo huu. Na taasisi ambayo anaiongoza mkurugenzi mwenye udhibiti mwenye kujali, sifa hiyo inatawala mazingira yake na inawadhibiti wafanya kazi.

Hakika baadhi ya wakurugenzi na viongozi katika idara na taasisi wanahesabu nafsi zao kuwa wako juu ya kanuni na sio wenye kuwajibika na kanuni, lakini wao wanawabana wafanyakazi kufuata nidhamu na kanuni, kwa kweli mchanganyiko huu hauleti matunda isipokuwa kufeli katika kazi na uhusiano mbaya baina ya idara na wafanyakazi. Anasema Mwenyezi Mungu swt.:

أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنسَوْنَ أَنفُسَكُمْ وَأَنتُمْ تَتْلُونَ الْكِتَابَ

**"Je, mnawaamrisha watu kutenda mema na mnajisahau hali mnasoma Kitabu?"** (Sura al-Baqarah: 44).

Na anasema tena:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٢﴾ كَبُرَ مَقْتًا عِندَ اللَّـــهِ أَن تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ

**"Enyi mlioamini! Kwa nini mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa kwa Mwenyezi Mungu kusema msiyoyatenda." (Sura Saf: 2 – 3).**

Ni mazuri sana yale aliyoyausia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwa Abdullah bin Mas'ud, alimwambia: "Ewe Ibnu Mas'ud usiwe miongoni mwa wenye kuwabana watu na kufanya tahafifu katika nafsi zao, Mwenyezi Mungu anasema: **Je, mnaamrisha watu kufanya wema na mnazisahau nafsi zenu.** Ewe Ibnu Mas'ud, usiwe kati ya wanaoongoza watu kufanya kheri na wanaamrisha kheri na wao wanaghafilika kuitenda, Mwenyezi Mungu anasema: **Je, mnaamrisha watu kufanya wema na mnasahau nafsi zetu.**"[62] Na anasema Imam Ja'far as-Sadiq (as): "Kuweni wenye kuwalingania watu kwa vitendo vyenu." [63]

[62] al-Majilisiy: Muhammad Baaqir katika *Biharul-Anwar*, Juz. 74, Uk. 109 - 110.

[63] Al-Hakiym: Muhammad Ridhwa – Muhammad – *Ali katika al-Hayatu*, Juz. 1, Uk. 326.

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA

## AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr

20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita

70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali

95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102 Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano

121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu

145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Mshumaa.
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka

170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
185. Kazi na bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Weledi juu ya Mustakabali
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
192. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
193. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
194. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)

195. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
196. Takwa
197. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu

## KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi